# KUISHIRIKI IMANI YAKO



4

Kutoka kwa Mfululizo: Hatua Kuelekea Ukomavu

Barry St.Clair



**Barry St. Clair** anatamani kuwaathiri vijana wengi iwezekanavyo kumfuata Kristo. Kama rais wa Reach Out Youth Solutions, yeye huongea kwa maelfu ya wanafunzi kila mwaka na ni mwandishi wa vitabu Zaidi ya 20, vikiwemo mfululizo wa vitabu vya Hatua Kuelekea Ukomavu. Barry huzuru ulimwengu kote akiwafunza viongozi wa vijana, wazazi na wanafunzi. Kupitia kwa uongozi wake, maelfu ya makanisa yameiga mkakati wa Huduma ya Vijana Inayomlenga Yesu.Barry amewahi kuichezea timu ya 3 ya mpira wa vikapu Marekani na ameshiriki kukimbia mbio za Boston Marathon. Yeye na mke wake Lawanna, wana watoto wanane na wanaishi Atlanta Georgia.

## VITABU VYA HATUA KUELEKEA UKOMAVU (VITABU ZAIDI YA 1,000,000 VIMECHAPISHWA)

Rafiki zako watampataje Yesu? Kupitia kwako! Kuishinda hofu ya kukataliwa na kupata Imani ya kulinena jina la Yesu kwa ujasiri kuna hatari zake. Kujihatarisha kwa kumwasilisha Yesu kutakuongoza na kukuelekeza katika safari za uwindaji. Kitabu hiki kitakuwezesha Kumfuata Yesu unapo:

- Ona mahitaji ya watu
- Shinda uoga
- Vumbua ujasiri
- Wafanya marafiki kwa ajili ya Kristo
- Anzisha mazungumzo
- Hadithia hadithi yako
- Wasilisha ujumbe
- Waelekeza marafiki kufanya uamuzi
- Jibu maswali magumu
- Msaidia mwamini mpya kukua

Vitabu vingine katika mfululizo wa vitabu vya *Hatua Kuelekea Ukomavu* ni:

- Kuanza
- Wakati wa Pekee na Mungu
- Kuuathiri Ulimwengu wako
- Kumfuata Yesu
- Kumfanya Yesu Bwana
- Kitabu cha mwongozo
- wa Wakati Pekee na Mungu
- Miongozo ya Viongozi

# KUISHIRIKI IMANI YAKO

KUTOKA KWA MFULULIZO WA VITABU VYA

## HATUA KUELEKEA UKOMAVU

**BARRY ST. CLAIR**

**kuishiriki Imani Yako**

ISBN: 9781610472555
© 2011 na Barry St. Clair. Haki zote zimehifadhiwa.
Imechapishwa na Wino wa NOVO - www.novoink.com

Toleo la kwanza na la Pili lililochapishwa na Reach Out Youth Solutions, 1991 na 2002.
Manukuu yote ya Biblia, imeonyeshwa vinginevyo, yametoka katika Biblia Takatifu, New International Version. © 1973, 1978, 1984, International Bible Society. Inatumiwa kwa ruhusa ya Zondervan Bible Publishers. Nukuu nyingine ni kutoka katika King James Version (KJV).
Hakuna sehemu nyingine ya kitabu hiki inayoweza kunakiliwa bila idhini iliyoandikwa, isipokuwa kwa manukuu mafupi katika vitabu na mapitio muhimu.

# YALIYOMO


Kutoka kwa Mwandishi 5

Kusudi 7

Matumizi ya Kitabu Hiki 8

Vidokezo vya Vitendo 9

Ikiwa uko kwenye Kikundi cha Uanafunzi 10

Ahadi ya kibinafsi 11

1 POTEA! 12

Kuona hitaji

2 KUTOKA HOFU HADI IMANI 23

Kushinda

3 NGUVU YA AJABU 35

Ujasiri katika Roho

4 RAFIKI MWENYE UHITAJI 48

.kutengeneza (au kristo

5 HUSIANA NA WASILIANA…………………. .62

Kuanzisha mazungumzo

6 UGUNDUZI WANGU MKUBWA……………. 71

Kutoa ushuhuda wa kibinafsi

7 UJUMBE …………………………………….. 80

Kuwasilisha ukweli o( Injili

8 CHORA WAVU………………………………. 93

Kuongoza (huenda kwa uamuzi

MASWALI 9 MAGUMU……………………… 102
Kujibu maswali wanayouliza wasioamini

10 KUANZA………………………………….. 118
.kumsaidia mwamini mpya kukua

Kadi za kumbukumbu za Biblia………………. 127

## SHUKRANI ZA PEKEE

Kwa Rod Minor na Debbie Hayes kwa kufanya kazi katika mradi huu pamoja nami.

Kwa Burt Stouffer na Ernest Pullen kwa kubuni na kufungasha mfululizo wa vitabu vya Hatua Kuelekea Ukomavu.

Kwa mke wangu marehemu Carol na watoto wangu Scott na Cameron, katie na Bart, Jonathan na Ginny ambao wamenipenda na kunitia moyo katika huduma yangu.

Kwa Lawanna. mke wangu, mpambanaji mwenzangu katika mauti na uzima na mwenzi wa moyo wangu kwa nusu ya pili ya maisha yangu.

Kwa Bwana Yesu Kristo kwa kunifundisha kweli halisi katika kitabu hiki.

# NENO KUTOKA KWA MWANDISHI

Watu wameeleza umuhimu wa kuishiriki imani yetu katika njia mbalimbali:

- Kuwaambia watu juu ya Yesu Kristo ni jambo kuu tangu zama za wakati siagi ya njugu karanga ilipoandaliwa kwa mara ya kwanza.

- Kushuhudia ni 'ombaomba' mmoja mwenye njaa akimwambia 'ombaomba' mwingine mwenye njaa wapi watapata mkate.

- Maisha ya Kikristo bila kushuhudia ni kama kula viazi baridi vilivyopondwa.

Lakini Mtume Paulo alieleza vizuri zaidi, "Siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila mtu aaminiye; kwanza kwa Myahudi, kisha kwa Myunani" (Warumi 1:16).

Mara tu baada ya kumkubali Yesu Kristo, nilisimama kanisani nikiwa na jasho kwenye viganja vya mikono na huku moyo unanidunda na kuwaambia watu kanisani kwamba nilimwalika Yesu kuishi ndani yangu. Niliwaambia nilitaka Warumi 1:16 iwe kweli kunihusu. Nilitaka kuwa shahidi asiye na haya wa Yesu Kristo. Tangu wakati huo, kumuwasilisha Kristo kwa watu wengine kumethibitika kuwa jambo la kusisimua

Kuwasiliana kuhusu imani yetu hutuchochea kukua katika imani yetu. Kiitabu hiki kiitakusaidia kuwa Mkristo wa Warumi 1:16 – asiyeionea haya Injili. Ninakupa changamoto kuungana nami katika fursa na changamoto ya kila siku ya kuishiriki imani yetu.

Mfululizo wa vitabu vya *Hatua Kuelekea Ukomavu* unajumuisha vitabu vitano vilivyoundwa kukusaidia kukua katika Kristo na kutoa maisha yako kwa wengine.

Kwa kupitia; *Kumfuata Yesu, Kutumia Muda Peke Yako na Mungu*, na *Kumfanya Yesu kuwa Bwana* utakufanya kuwa na ufahamu thabiti wa

Mungu ni nani na wewe ni nani katika Kristo. Sasa ni wakati wa kuwazingatia watu wengine. Wao, kama sisi, wana hitaji kubwa kwa ajili ya Yesu na ndani mwao mna hamu kubwa sana ya kumpata. Mungu anataka kukutumia kuwatia moyo ili wamjue.

Baada ya kukamilisha kitabu hiki, maliza mfululizo kwa kupitia *Kuuathiri Ulimwengu Wako*.

Matamanio ya Mungu na maombi yangu kwako ni kwamba mambo utakayoyavumbua katika kurasa zinazofuata hazitakuwa sehemu ya madokezo yako tu, bali sehemu ya maisha yako. Naomba yote yatakayokamilishwa katika maisha yako yawe kwa ajili ya heshima na Utukufu Wake.



# KUSUDI

Kitabu hiki kitakusaidia kufahamu mojawapo ya misingi ya kuishi maisha yako na Yesu Kristo. Utagundua nafasi yako katika mpango wa Mungu wa kuwaongoza watu kwake Mwenyewe. Kupitia kile utakachojifunza, utafanya hatua inayofuata kuelekea njia ya uanafunzi wa kweli.

Uanafunzi unaweza kufafanuliwa kwa kiasi kama:
- -kuwa huru kumtegemea Yesu Kristo, na
- -kuwafundisha watu kufundishwa na Mungu.

Paulo alitoa muhtasari wa mchakato wa ufuasi wa kibinafsi aliposema, "Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu;" (Wafilipi 1:6).

Kabla ya kuanza kufanya mafunzo ya Biblia katika kitabu hiki, mwombe Yesu Kristo ayakamilishe yote anayotaka kufanya maishani mwako.

# MATUMIZI YA KITABU HIKI

1. MAKUNDI MADOGO: Unaweza kutumia kitabu hiki kama mwanachama wa kikundi kilichopangwa (Kikundi cha Wanafunzi) kikiongozwa na kiongozi mtu mzima. * Kila mmoja katika kikundi hiki anatia saini karatasi ya ahadi kwenye ukurasa wa 11, na anakubali kutumia kitabu hicho wiki baada ya wiki kwa ukuzi wa kibinafsi.

2. WATU BINAFSI : Unaweza kupitia kitabu hiki peke yako, ukifanya somo moja kila wiki kwa ukuaji wako binafsi.

3. KUWAFUASA WANAFUNZI WACHANGA : Baada ya kufanya kila kipindi katika kitabu hiki kuwa sehemu ya maisha yako mwenyewe, unaweza kumsaidia kijana au kundi la vijana kupitia kitabu cha *Kuishiriki Imani Yako*.

---

*Mwongozo wa Kiongozi wa Mfululizo wa vitabu vya *Hatua kuelekea Ukomavu* unaweza kununuliwa kutoka kwa *Reach Out Youth Solutions*. Tazama maelezo ya agizo nyuma ya kitabu hiki..

## VIDOKEZO VYA UTENDAJI

(Jinsi ya kupata manufaa zaidi kutoka kwa kitabu hiki)

Ikiwa unataka kukua kama Mkristo, lazima uwe mhalisi na Mungu na uitumie Biblia kwa maisha yako. Wakati mwingine ni vigumu, lakini kitabu hiki kinaweza kukusaidia ikiwa utatamani.

1. Anza kila kipindi kwa maombi.
Mwombe Mungu aseme nawe.

2. Tumia Biblia ambayo ni rahisi kusoma.
Jaribu New International Version.

3. Pitia katika kipindi kizima.

- Tafuta mistari ya Biblia.
- Tafakari kupitia majibu.
- Andika majibu.
- Andika maswali yoyote uliyo nayo.
- Kariri aya uliyopewa.

(Tumia kadi za kumbukumbu za Biblia nyuma ya kitabu.
Vikundi vinapaswa kuchagua tafsiri moja kwa kukariri, ili kukariri aya pamoja.)

4. Tumia kila sehemu maishani mwako.

- Mwombe Mungu akuonyeshe jinsi ya kutenda kulingana na jinsi ulivyojifunza kutoka kwa Neno lake.
- Mtii Mungu katika mahusiano, mitazamo, na Vitendo vyako.
- Zungumza matokeo na waumini wengine wanaoweza kukuhimiza na kukushauri.

## IWAPO U KATIKA KIKUNDI CHA UANAFUNZI

- Tenga nyakati mbili tofauti kila juma ili kufanyia kazi uliyopewa katika kila kipindi. Ikiwezekana, kamilisha somo lote la Biblia wakati wa mara ya kwanza. Kisha wakati wa pili (siku ya au siku kabla ya mkutano wako ujao wa kikundi), kagua kile umejifunza.

- Chukua Biblia yako, kitabu hiki, na kalamu au penseli kwa kila mkutano  wa kundi.

## KUJITOLEA BINAFSI

**Mimi, ---------------------------------------- , najitolea kwa ahadi zifuatazo:**

**1. Kujitoa kila siku kwa Mungu na kwa yote ambayo anataka kunifundisha kuhusu kukua kama mfuasi wa Yesu.**

**2. Kuhudhuria mikutano yote ya kila wiki ya kikundi isipokuwa ugonjwa mbaya au hali kama hiyo inafanya isiwezekane. Ikiwa nitakosa zaidi ya mkutano mmoja, nitajiondoa kwa hiari kutoka kwa kikundi ikiwa itakuwa muhimu baada ya kukutana na kiongozi wa kikundi.**

**3. Kumaliza kazi bila kukosa kwani zinastahili kuwa tayari kila wiki.**

**4. Kushiriki kikamilifu katika kanisa langu.**

**Ninaelewa kuwa ahadi hizi sio kwa Bwana Mungu tu bali kwa kikundi na kwangu pia. Kwa msaada wa Mungu, nitajitahidi kadiri niwezavyo kutimiza kila moja.**

**Saini______________________ Tarehe___________________**

# SEHEMU YA 1




## Kuiona Haja

Jumatano iliyopita usiku, kiongozi wa vijana wa Andy alizungumza na kundi lao kuhusu kuiwasilisha imani yao. Alitoa changamoto kwa kila mtu kueleza imani yake kwa mtu mmoja katika wiki ijayo. Andy mara moja alimuwazia rafiki yake, Yohana.

Yohana anatoka katika familia inayoheshimika. Baba yake ni mkwasi wa pesa kwa kazi yake. Wazazi wake wameoana kwa furaha. Yohana ana marafiki wengi na anapatana pamoja nao shuleni. Ana kila kitu na mambo yake yanamwendea vizuri. Lakini Andy hana uhakika kuwa Yohana ni mfuasi wa Yesu na hata anashangaa kwa nini Yohana angemhitaji Yesu Kristo. Ungempa Andy ushauri gani?.

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

Unapofikiria kuishiriki imani yako, ni picha gani ya kiakili unapata?

-> Kukigonga kichwa cha mgeni kwa Biblia yenye uzito wa pauni 50?.

-> Kuwaambia marafiki zako wanaenda kuzimu?

-> Umesimama kwenye kona ya barabara, ukihubiri juu kabisa ya mapafu yako?

-> Kutawanya trakti kwenye chumba chote cha chakula cha mchana?.

Ikiwa neno shahidi linatoa taswira yoyote kati ya hizo hapo juu, wewe pengine hauna msisimko sana kuhusu kuishiriki imani yako. Labda wewe haujali. Unaogopa marafiki zako watafikiria

nini. Lakini hebu angalia kuishiriki imani yako kwa mtazamo mwingine.
Fikiria kwenda kuogelea na marafiki zako. Unapumzika ufukweni wakati mmoja wa marafiki zako anapata mkorogo wa tumbo na anajipindapinda. Kihifadhi maisha ki karibu nawe. Mwitikio wako ni upi? Je, umezimwa na kujawa na kutojali, au kuogopa sana kuchukua hatua? Je, utaanza kujiuliza kama huyo mtu atajali ikiwa utaokoa maisha yake? Hapana! Silika zako zinakuambia ufanye chochote unachoweza ili kumuokoa rafiki yako. Kushuhudia ni kushiriki Injili (mhifadhi uhai; Yesu Kristo) pamoja na marafiki zako ili kuwaokoa kutokana na kifo cha kiroho na kuwapa uhusiano wa ajabu wa kibinafsi na Yesu sasa na hata milele.

### WEMA. WABAYA. WALIOPOTEA

Biblia inaeleza mtu asiye na Yesu Kristo kuwa amepotea (Luka 19:10).
Eleza tukio katika maisha yako ulipopotea. Ulijisikiaje?
________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________
______________________

**Katika Matendo 3:1-10** tunasoma juu ya mtu ambaye anaashiria upotevu wa binadamu. Soma kifungu kisha zingatia ukweli Ufuatao kuihusu hali yake..

**1 Mtu Huyo Alikuwa Kilema (Matendo 3:2)**

Mwanamume huyo, kilema tangu kuzaliwa, alikuwa na mahitaji makubwa sana. Alikuwa amepotea lakini hakujua. Ingawa alikuwa anaishi katika kivuli cha hekaluni, alikuwa na dini ya kutosha tu kumfanya asimjue Mungu wa walio hai.

Je, umetambua kwamba watu wengi waliopotea ni wa kidini kwa kiasi fulani? Wanaamini katika jambo fulani. Wana mungu wa namna fulani. Wengine wanaishi kwa maisha. Lakini ni vilema—ama kihisia-moyo, kimwili, au

kiroho—na hawawezi kuyakidhi maisha yao.

Fikiria mtu unayemjua ambaye anaonekana kufaa "kidini, lakini amepotea". Mfafanue hapa chini.

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

**2 Huyu kilema alikuwa na upungufu (Matendo 3:3)** Mtu huyu alijua jinsi ya kuomba. Aliishi kila siku akijaribu kupata pesa za kutosha kuishi. Kwa sababu ya mtazamo wake mdogo mwenyewe, hakujua yeye ni nani au angeweza kuwa nani. Kama mtu huyu, wanafunzi wengi wana maoni machache kuhusu maisha yao. Wanaota kupata magari mapya, stereo mpya, nguo zinazofaa, na vitu vingine vya kimwili. Bado wanaonekana kutomjali Mungu. Wakati mwingine tunawaangalia hao watu na kufikiria, "natamani ningekuwa na walichonacho". Tunaweza hata kujaribiwa kufikiria kuwa hawamhitaji Mungu. Lakini ijapokuwa wana miungu vibadala vya Mungu katika maisha yao, wao wamepotea. Hawatakuwa na uzima bila kumjua Yesu Kristo na kukua katika uhusiano imara naye.
Eleza mmoja wa marafiki zako ambaye ana maoni machache kujihusu na maisha yake.

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

**3 Kilema huyu mwenye upungufu alikuwa yuatazama (Matendo. 3:3-5)** Petro na Yohana walipomwambia yule kiwete kuwatazama, 'aliwapa usikivu wake.' Alitazamia kupokea kitu fulani, alikuwa akiangalia...akitafuta...akitumainia kitu bora zaidi siku zijazo.

Watu wengi shuleni kwako wanatafuta kuridhishwa na wanachofanya au walichonacho. Ni nani mtu mmoja wewe unayemjua ambaye anatafuta kitu bora zaidi? Yeye ni kama nani au nini?

_______________________________________________

Hebu tuchunguze kwa undani zaidi jinsi mtu asiye na Yesu Kristo alivyo.
--Kiroho (amelemazwa na hatia na anaogopa kifo)
--Akili (hupata kujistahi chini na kuchoka na maisha)
--Kihisia (ana upweke unaoumiza na upendo usio na imani)
--Kijamii (hufanya kwa mafanikio, hujaribu kujithibitisha, na kujiweka yeye mwenyewe kwanza)

Huyu mtu ana sifa hizi tatu si kwa sababu ya kile anachofanya, lakini ni kwa sababu yeye ni nani - mtu asiye na Yesu Kristo katika maisha yake. Mtu huyo anaweza kuonekana kama mtu aliyepotea kabisa au kuonekana kama yeye ana kila kitu. Anaweza kuwa na "mashimo" kiadili au anaweza kuwa na maadili ya hali ya juu kupita viwango na hata kuhudhuria kanisa mara kwa mara. Kwa vyovyote vile, mtu huyu ni kilema na mwenye upungufu katika kila eneo la maisha.

Ukizingatia orodha hii, angalia nyuma watu watatu ulioorodhesha hapo juu na uandike sentensi kuhusu kwa nini kila mmoja anamhitaji Kristo.

Jina Sababu

1. 

2. 

3. 

Tazama taswira ya watu watatu uliowaorodhesha nje ya bahari katika mashua yenye shimo kubwa ndani yake. Inazama. Wanahitaji mtu wa kuwaokoa au watazama. Hapo ndipo unapoingilia. Rafiki zako wamepotea; unao msaada wanaouhitaji.

**Soma Luka 15**. Mifano ya Biblia mitatu inahusu mada moja.
Ni nini mada kuu ya sura hii?

Umegundua nini kutokana na kifungu hiki kuhusu mtazamo wa Yesu kuwaelekea watu waliopotea?


Yesu ana huruma kwa watu waliopotea. Anatupa changamoto kutamani kuwa na huruma Yake na kuwasaidia watu kutafuta njia ya kumuelekea.

**KUWAPENDA WATU WALIOPOTEA**

Sasa tunaelewa kwamba watu wasio na Kristo wamepotea, na kwamba Mungu anataka kutupa huruma kwa ajili yao, tunawezaje kuwasaidia kupata njia yao kwa Kristo? Hebu tuone Petro na Yohana walifanya nini.

**Soma tena Matendo 3:6-10**. Petro na Yohana walisimama tayari kumsaidia kiwete huyo kwa njia yoyote ile. Petro akamwambia, "Nilicho nacho hicho ndicho ninakupa (Mst.6).

Mtazamo ulioje! Wawezaje kuukuza mtazamo wa upendo kwa wengine kama mtazamo wa Petro na Yohana?




**1 Ukweli wa Upendo wa Yesu Kwako**

Upendo kwa watu hutokea unapoelewa jinsi Yesu Kristo alivyo muhimu kwako binafsi. Petro na Yohana walikuwa wameshuhudia upendo wa Yesu walipokuwa wamepotea na kutopendwa. Miaka mingi baada ya Petro na Yohana kumwona yule kiwete hekaluni, Yohana aliandika hivi: …"Tunawahubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu; hilo tulilolona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi: nana ushirika wetu ni na na ushirika wetu ni pamoja na Baba na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo. Na haya twayaandika, ili furaha yetu itimizwe. (1 Yohana 1:2-4).

Upendo wa Yesu ulikuwa wa kweli sana kwa Petro na Yohana. Je, upendo wa Yesu ni kweli kwako wewe? Ni lini umepata uzoefu kwamba Yesu anakupenda hata wakati

wewe haupendeki?

## 2 Usadikisho Kwamba Yesu Ndiye Jibu la Mwisho kwa Uhai

Je, una hakika kwamba watu bila Yesu Kristo wamepotea - wanaishi nje ya uwepo wa Mungu sasa na hata milele?

> Michael Green alisema: "ikiwa unaamini hivyo Kwamba nje mwa Yesu Kristo hakuna matumaini, haiwezekani kumiliki hata chembe moja tu ya upendo na fadhili bila kushikwa na hamu kubwa ya kuwalete watu kwa njia hii moja ya wokovu"
> *(Evangelism in the Early Church, Eerdmans, p.249).*

**Soma Mathayo 25:40**. Yesu alisema nini kuhusu usadikisho wa mwamini kuwasaidia watu waliopotea? Unafikiri Alimaanisha nini?

**Kulingana na Matendo 4:10-12**, kwa nini hakuna "wokovu..katika mtu mwingine" isipokuwa Yesu Kristo?

Unaposadikishwa na ukweli huu, utataka kuwapa marafiki zako upendo wa Yesu.

Ikiwa huna hamu hii ya kuona watu waliopotea wakimjua Kristo,
jiulize kwanini hauna hiyo hamu:

--Je, ninamwasi Mungu?
--Je, nina dhambi yoyote ambayo haijaungamwa?
--Je, kuna jambo lolote maishani mwangu lililo muhimu zaidi kumliko Yesu?

## 3 Tabia ya kuishi Katika Uwepo Wa Yesu Kila Siku

**Soma Matendo 4:13**. Kuishi katika uwepo wa Yesu kuliathirije

Petro na Yohana?

kuishi kila siku katika uwepo wa Yesu, kutakupa ujasiri wa kuwaambia rafiki zako kumhusu Kristo.

Fikiria wazo moja la ubunifu, la vitendo ili kukukumbusha kuwa wewe waishi katika uwepo wa Yesu kila dakika ya siku..

## DONDOO ZA KUWAPENDA WATU WALIOPOTEA

Kwa wakati huu unaweza kuwa unafikiri, mimi sio Petro au Yohana. Uko sawa, lakini wewe ni wewe. Kwa kuwa unamjua Yesu na umejazwa na Roho Mtakatifu, wewe unacho kile kinachohitajika kuwapenda watu waliopotea. Mungu tayari ameweka upendo wake ndani ya moyo wako. Sasa unahitaji kujifunza kuupitisha kwa wengine.

Unauonyeshaje upendo wa Kristo kwa mtu aliyepotea?

> **Kama naujua upendo wa Kristo...**
> **na ikiwa namjua mtu aliyepotea ...**
> **basi naweza kueleza upendo**
> **wa Kristo kwa mtu huyo.**

**1 Wajue Watu Waliopotea**
Yule kiwete hakuweza kuwaendea Petro na Yohana, kwa hiyo wakamwendea.

Vilevile, watu walio vilema wa kiroho hawatatujia pia. Mara ya mwisho ilikuwa lini mtu alikuja kwako na kukuuliza jinsi wanavyoweza kumjua Yesu. Sisi ni lazima kwenda kwao. John Stott anaelezea "Wakristo wa shimo la sungura" ni kama hao ambao wako karibu sana na watu wasio Wakristo siku nzima, lakini hawajawahi kuwashirikia Kristo. Wao huchomoza vichwa vyao kutoka katika nyumba zao za Kikristo kila asubuhi na kukimbilia darasani, ili tu kutafuta marafiki wa Kikristo wa kuketi karibu nao. Shuleni wanatoka darasa hadi darasa, kisha wanajipanga tena mkahawani kwa kile wanariadha huita "kusanyiko takatif u" (kona ya Wakristo wote). Na wakati huu wote Wakristo

wanafikiri. Ni ushuhuda wa namna gani huu! Usiku unapofika, wanaenda kwa somo lao la Biblia la Wakristo pekee ambapo pengine watasali kwa ajili ya wasioamini. Kisha wanakimbilia nyumbani, wakiwa na furaha kuwa salama mchana kutwa bila kupata manyoya yao kuchafuliwa na ulimwengu! (Kutoka katika kitabu cha *Out of the Salt Shaker*, Rebecca Manley Pippert, InterVarsity Press, uk. 124)

Je, unaweza kujieleza kama "Mkristo wa shimo la sungura"?.

Ni kwa njia zipi "unakutana" na watu waliopotea?

Taja rafiki mmoja ambaye unadhani anahitaji kumjua Yesu Kristo.

**2 Kusudieni kuwa na nia moja**

Petro na Yohana walianzia pale ambapo yule kiwete alikuwa ametaka kupata pesa. Wao waligeuza tamaa hiyo kuwa fursa ya kuzungumza naye kumhusu Yesu.

Ni nini moja ya maslahi ya rafiki yako ambaye amepotea? (Fikiria kuhusu mambo ya kufurahisha, michezo, safari, vitabu, marafiki wengine, n.k.)

**3 Kutana na hitaji la huyo mtu mwingine**

Yule kiwete alifikiri anataka pesa, lakini alitaka sana kutembea. Petro na Yohana walitimiza uhitaji huo na kumponya yule mtu kilema.

Unafikiri ni hitaji gani la kweli la rafiki yako aliyepotea? Ni vipi unaweza kukidhi hitaji hilo haswa?

> **Haja kubwa sana ambayo wewe unaweza kutimiza ni kumuongoza rafiki yako kwa Yesu Kristo**

**4 Mfanye Yesu kuwa suala lako.**
Petro na Yohana hawakumzingatia mtu yule kiwete au uponyaji wao wa muujiza. Mtazamo wao ulikuwa kwa Yesu Kristo.

Unawezaje kumfanya Yesu kuwa suala kwa rafiki yako?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

> **kama maswali ya awali yalikuwa magumu kujibu, usijali.Sehemu nyingine yote ya kitabu hiki iliyosalia inalenga kukupa njia maalum za kuwapenda marafiki zako nakuwaongoza kwa Yesu**




**Watu** sio nafsi za kufikirika tu ili kuokolewa. Hawatakujibu hadi wamekujua wewe na nia yako ya kweli kuwahusu. Watu wanaojaribu kuwasiliana na Kristo bila mtazamo wa upendo, huwasilisha Ukristo kama kitu cha kuepukwa. Lakini upendo wa Yesu ukiwa hai ndani yako atawahuisha rafiki zako ambao bado si waumini.

Wiki hii tumia vidokezo vitano katika somo hili la Biblia ili kupata uhusiano wa undani zaidi na rafiki yako asiyeamini

1. Amua ni nani utamtolea upendo wa Yesu wiki hii.

2. Kutana na mtu huyo kwa wakati wa kufurahi pamoja. Barizi naye kwa soda au vitafunaji.

3. Gundua mahitaji yake. Mwambie hitaji lako kuu, kisha muulize hitaji lake ni lipi.

4. Wakati wa mazungumzo yako, taja jina la Yesu angalau mara moja.

5. Mwombee. Mwombe Yesu ajidhihirishe halisi kwake.

**Kamilisha kipindi hiki kwa kukariri Yohana 17:3.**

## KAZI

1. Kuwa na wakati peke yako na Mungu kila siku wiki hii, kwa kufuatia usomaji ufuatao wa Biblia.

Siku ya 1: Matendo 1:1-11

Siku ya 2: Matendo 1:12-36

Siku ya 3: Matendo 2:1-13

Siku ya 4: Matendo 2:14-28

Siku ya 5: Matendo 2:29-47

Siku ya 6: Matendo 3:1-10

Siku ya 7: Matendo 3:11-36

**2. Kamilisha Sehemu ya 2.**

3. Rudia mistari yote ambayo umejifunza kama ulijifunza *Kumfuata Yesu, Kutumia Muda Peke Yako na Mungu, na Kumfanya Yesu kuwa Bwana*. Jifunze maneno haya kamili ili kumwambia mwenzio wiki ijayo.

4 Kuja pamoja na rafiki asiye Mkristo na ufuate maagizo
yaliyotolewa katika somo hili la Biblia.

# SEHEMU YA 2




# KUSHINDA HOFU

Andy humwona rafiki yake Yohana kila siku katika darasa la Kiingereza. Andy anataka kumuelezea Yohana kuhusu uhusiano wake na Yesu. Lakini Andy anaogopa. Kama ungekuwa wewe Andy, ungeogopa? Kwa nini?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Ikiwa unaogopa kuwaambia wengine kumhusu Kristo, je, unapaswa kupuuzilia mbali tu? Je, inaweza kweli kuwa muhimu hivyo?

**Katika 1 Yohana 1:3-4**, Yohana, mfuasi wa Yesu, alikuwa na sababu nzuri za kuwaambia wengine kuhusu Yesu. Zilikuwa zipi?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Fikiria umekaa kwenye chakula cha jioni. Mama yako ameweka mnofu wa nyama, yenye utamu, mkate uliookwa nyumbani na siagi iyeyukayo pole, keki ya chokoleti ya kupendeza... na viazi baridi vya kupondwa! Yuk!
Paul Little anasema, "Maisha ya kikristo bila kushuhudia ni kama kula viazi vilivyopondwa" (*Jinsi ya Kushiriki Imani Yako*, InterVarsity).

Usipowaambia wengine kuhusu Yesu, maisha yako ya

Kikristo kamwe "hayataonja" ladha. Yatakuwa na ladha ya viazi baridi vya kupondwa.
Hata hivyo kujua hilo hakuondoi hofu zetu. Na hofu zetu zinaelekea
kutupooza na kutufanya tusifanye lolote.Tunawezaje kushinda woga wetu?

## HOFU INAWEZA KUJENGA IMANI YETU

> **Hofu ni sawa kama inatufundisha kumtegemea Kristo.**

Hofu ni jambo la kawaida. Nimezungumza na watu kumhusu Yesu Kristo kwa zaidi ya miaka 30, na bado ninapata hofu. Sio vigumu sana kuzungumza juu ya michezo au shule, lakini watu mara nyingi huwa na wasiwasi mtu anapoanza kujadili masuala ya umuhimu wa kina wa kibinafsi.

**Katika 1 Wakorintho 2:1-5** jinsi gani Paulo alikabiliana na hofu yake.

Tatizo la Paulo lilikuwa nini? (Mst.3)

Ni nini kilichomfanya Paulo ashinde woga wake? (Mst.2)

Woga huo ulifanya nini kwa uwezo wa Paulo wa kushuhudia Kristo? (Mst. 4)

Hofu hiyo ilimfanya Paulo kuitikia “si katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu” (mstari 5) Tunapokuwa na woga, tunaweza kukua katika imani yetu kama sisi tutakabiliana na hofu hizo na kumwamini Kristo na uwezo wake wa kuzishinda.

## HOFU INAWEZA KUIDUMAZA IMANI YETU

Ikiwa tunaogopa na hatujifunzi kutegemea
Kristo, hofu yetu inakuwa mbaya. **Soma Yohana 20:19-22**. Ni vipi woga unailemaza imani ya wanafunzi?

> **Imani inaweza kushinda hofu yetu, lakini hofu inaweza kulemaza Imani yetu**

Jinsi gani imani ilishinda woga wa wanafunzi?

Baada ya Yesu kukamatwa na kusulubiwa, wanafunzi waliingia kinyemela kwenye chumba na kujificha. Hebu wazia tukio hilo. Milango imefungwa - imefungwa vizuri! Kila kelele kutoka nje huwafanya waruke. Wao wameogopa sana. Wanauma kucha kama
Kwamba wanazungumza. .wanaulizana, “Ni nini kitatokea sasa? Tutatokaje nje ya jiji bila kukamatwa? Pamoja na hadithi hizi zote kuhusu kaburi la Yesu kuwa tupu, wenye mamlaka hakika watatutafuta."

Wanafunzi walikuwa na sababu nzuri za kuogopa. Angalia mistari hii kuona kwa nini.

Mathayo 26:55-56

Luka 9:18-25

Yohana 18:19

**CHANZO CHA HOFU**

Wanafunzi hawakuwa na nia ya kutoka nje ya milango iliyofungwa kuzungumza juu ya Yesu Kristo! Hofu inaweza kuwa mbaya, ikituzuia kuchukua hatua ya kutenda lolote. Je, ni baadhi ya mambo gani yanayosababisha watu kuogopa kuzungumza kumhusu Yesu Kristo?.

**1 Hatia**

*Udhuru*: "Nina makosa mengi sana maishani mwangu. Ninaogopa kuwa mnafiki."

*Tatizo*: Kutojiona kuwa tunapendwa kabisa, tunakubalika, na tumesamehewa na Yesu. Tusipopokea kile Yesu alifanya msalabani tutahisi kuwa wenye hatia. Kadiri tunavyohisi hatia ndivyo tunavyoogopa kuzungumza na wengine kumhusu Yesu.

*Suluhu*: Kukubali upendo na msamaha wa Mungu.

**Soma Warumi 8:l; 1 Yohana 1:9–10**. Unawezaje kukabiliana na hatia?

**2 Shaka**

*Udhuru*: "Ninaogopa kuzungumza juu ya Yesu kwa sababu sina uhakika kabisa kuhusu uhusiano wangu na Yeye."

*Tatizo*: Kutojiamini. Ilimradi tuna shaka ya kibinafsi kuhusu uhusiano wetu na Kristo, hatutawahi kuwa na ujasiri kuhusu kumshirikisha na watu wengine.

*Suluhisho*: Uhakika. Biblia inaahidi kwamba tunaweza kuwa na uhakika katika uhusiano wetu na Yesu Kristo.

**Soma 1 Yohana 5:11-13** . Unawezaje kuwa na uhakika katika uhusiano wako na Kristo?.

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

**3 Uwezekano wa Kushindwa**
*Udhuru*: "Ninaogopa nitashindwa. Je, ikiwa mtu huyo hatampokea Kristo?"

*Tatizo*: Kuutegemea uwezo wetu. Tunapojitegemea nguvu zetu, tunaweza kuwa na uhakika kwamba tutashindwa. Ndiyo maana tunahitaji kuzitegemea nguvu za Mungu. Wajibu wetu si kuhakikisha kwamba watu wanampokea Kristo. Huo ni wajibu wa Roho Mtakatifu. Wajibu wetu ni kuwaambia wengine juu yake kwa uaminifu.

*Suluhu*: Nguvu za Roho Mtakatifu.

**Soma Isaya 41:10; Yohana 20-22**. Nguvu za Roho Mtakatifu zitakusaidieje kushinda woga wako wa kushindwa?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

**4 Kutojali**
*Udhuru*: "Sijali kabisa mahali ambapo watu wako na Mungu.
Kwani kuna jambo gani kubwa?"

*Tatizo*: Tamaa za ubinafsi. Tunajijali sisi wenyewe zaidi kuliko
kuwahusu watu wengine au matamanio ya Mungu. Hilo hutufanya tusimjali Mungu na watu wengine.

*Suluhu*: Matamanio ya Mungu.

**Katika Marko 4:19** Yesu anaeleza chanzo cha makosa mengi kuwa ni tamaa. Kulingana na mstari huu, unahitaji kufanya nini ili kuondoa hali ya kutojali inayokuzuia kumshiriki Kristo

## 5 Uwezekano wa Kuwaudhi Wengine

*Udhuru*: "Ninaweza kuvamia faragha ya watu wengine. Labda hata hivyo hawataki kujua. Sitaki kumuudhi mtu yeyote."

*Tatizo*: Mawazo yasiyo sahihi. Wakati fulani tunafikiri kwamba watu hawapendezwi na Yesu Kristo. Watu wengi hawafurahii Injili kusongwa kooni mwao, lakini kwa kawaida watu wanauthamini upendo unaowaelekea na uaminifu. Ukiamka usiku na kugundua kuwa nyumba ya jirani yako imewaka moto, ungefanya nini? Hungesema, "Sitaki kuvamia faragha yake kwa kumwambia kuwa nyumba yake inateketea kwa moto." Badala yake ungekimbilia nyumba yake, uupige mlangoni wake mpaka aamuke, na umjulishe kuwa nyumba yake inawaka moto. Matendo yako hayangekuwa ya kuudhi; wangeonyesha kujali kwako kwa dhati kwa mtu mwingine.

*Suluhisho*: Kujali.

**Soma 1 Wathesalonike 2:7-8**. Inagharimu aina gani ya kujali kutakaokufanya kushinda kusitasita kuhusu kumuudhi mtu?
Unawezaje kusitawisha kiwango hicho cha kuwajali wengine?

## 6 Ukosefu wa Maarifa

*Udhuru*: "Je, mtu akiuliza swali ambalo siwezi kujibu? Sijui
la kusema."

*Tatizo*:Kutojua. Je, tunashindaje kutojua kwetu kumhusu Mungu na Neno lake? Mtu anapotuuliza swali ambalo hatuwezi kujibu tunapaswa kukubali, kwenda kutafuta jibu, na kurudi kwake huyo mtu. Hiyo ni njia bora ya kujifunza.

*Suluhisho*: Uanafunzi.

**Soma Matendo 2:42** uone jinsi kanisa la kwanza lilivyoshinda
ukosefu wao wa maarifa. Orodhesha shughuli maalum ambazo wao
walifurahia.

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
______________________________

## 7 Kukataliwa

*Udhuru*: "Ninaogopa kile wengine watasema juu yangu
Watanicheka au kunadhani mimi ni mtu wa ajabuajabu’’

*Tatizo*: kujiona kuwa duni. Tafiti zimeonyesha kuwa asilimia 95 ya
wanafunzi wote hawajipendi kabisa. Miongoni mwa mambo mengine, wanataka kubadilisha sura zao, uwezo wao, na wazazi wao. Itakuwaje mtu ambaye tayari amejikataa mwenyewe kushiriki imani yake. Kwa nini mtu ambaye hajipendi yeye mwenyewe aujaribu mradi wa njia yake ya maisha juu ya mtu mwingine? Yeye
hawezi na hatafanya hivyo.

*Suluhisho*: Usalama.

**Soma Wakolosai 3:3** ili kugundua usalama wetu ulipo na jinsi tunavyoshinda hofu ya kukataliwa.

Tunapompokea Kristo tunakubaliwa naye kabisa kama mtoto wake. Kwa hiyo, tunapomshiriki Kristo na wengine hatuwezi kuumizwa na kukataliwa kwao kwa sababu tunajua kwamba kukubalika kwetu ni katika Yesu.

Kati ya chimbuko saba za awali za hofu, moja ambayo inakusababishia wewe shida zaidi ni ipi? Kwa nini?

**CHANZO CHA IMANI**

Hofu za wanafunzi zilishindwa kwa njia ya imani.

**Soma tena Yohana 20:19-22**. Kabla ya wakati huu wanafunzi
waliogopa kiasi cha kufa. Lakini baada ya mwezi mmoja hivi walikuwa wamesimama mbele ya watawala waliomhukumu Yesu auawe - watu wale wale waliokuwa wakiwawinda. Na sasa wakati wanafunzi walisimama mahakamani, walitangaza kwamba Yesu alikufa, alifufuka, na alikuwa yu hai. Waliiambia mahakama kwamba hawawezi kukana ukweli hata kama mahakama ilichagua kuwaua. (tazama Matendo 4:8-12).

Nini kilisababisha mabadiliko kutoka kwa
hofu na kuleta kujiamini, kuwa na nguvu, ujasiri, shauku, na furaha?

**Imani yetu kumshiriki Kristo ni hofu ambayo imechukua na kuubeba Msalaba.**

Yesu Kristo anaweza fanya mabadiliko ya aina hiyo katika maisha

yako pia. Angalia vyanzo vya imani vifuatavyo kutoka **Yohana 20:19-22** ili uweze kujifunza kuushinda woga katika kuishiriki imani yako.

**1 Uwepo wa Yesu**
"Yesu akaja akasimama kati yao" (Yohana 20:19). Tangu ufufuo, uwepo wa Yesu umekuwa na na sisi siku zote

**Soma Mathayo 28:19-20**. Ni mara ngapi na kwa muda gani uwepo wa Yesu utakuwa pamoja nasi?

**2 Amani ya yesu**
“Amani iwe nanyi,” Yesu asema (Yohana 20:19). Baada ya kumkana Yesu, wanafunzi walitazamia kuwa atawashutumu kwa kumkana. Badala yake, Yesu aliwapa amani yake. Kwa nini? Kwa sababu hukumu na hatia si sehemu ya maisha ambayo Yesu anataka wafuasi wake waishi. Yeye hutupa amani yake ili kushinda wasiwasi na woga.

**Soma Yohana 14:27**. Jinsi gani ahadi ya Yesu ya amani inatumika
kwako?

**3 Mpango wa yesu**
“Kama vile Baba alivyonituma mimi, nami nawatuma ninyi” (Yohana 20:21). Dhamira ya Yesu ni dhamira yetu. Kama vile Baba alivyomtuma ulimwenguni kutangaza injili, anatutuma katika ulimwengu wetu kufanya vivyo hivyo. Tunapowaambia wengine kumhusu Yesu, tunaweza kutarajia kukataliwa na watu fulani. Kwa kweli, neno la Kigiriki kwa shahidi (marturia) ni neno moja sisi
tunalitafsiri kama "shahidi," au mtu anayekufa kwa sababu ya anayoamini sana.

**Soma Luka 9:23-26** Je, unawezaje kujiandaa kukabiliana na kukataliwa?

Ingawa watu fulani kwa hakika watakataa ujumbe wetu, wengine wataupokea. Huenda tukafikiri kwamba watu hawatapendezwa na ujumbe tulio nao, lakini watu wengi wana hamu ya kumjua Yesu Kristo. Tunaweza pia kuutegemea ukweli kwamba Mungu anafanya kazi katika maisha ya watu wengine hapo awali kabla ya sisi kuanza kuzungumza nao.

Soma Matendo 2:37-41. Baada ya Mungu kuitayarisha mioyo ya
watu kwenye Siku ya Pentekoste, walifanya nini kuutikia ujumbe wa Petro?

## 4 **Kupenya kwa yesu**

Yesu alisema, "Pokeeni Roho Mtakatifu" (Yohana 20:22) Wanafunzi walimjua Yesu kwanza kwa nje, lakini walipopokea
Roho Mtakatifu, walianza kumjua kwa undani.
Roho wa Mungu alileta tofauti yote, kwa sababu Yeye aliyapenya maisha yao. (**tazama Wakolosai 1:27-28**.)

> **Hamu ya mungu ya kuwafikia watu ni kubwa zaidi kuliko hofu yetu.**

Si tu kwamba Yesu yuko pamoja nasi na ndani mwetu, bali pia Anatoa nguvu kwa ajili yetu - Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hutufanya tuwe na ujasiri, hutupatia hekima na ufahamu, hubomoa ulinzi wa mtu mwingine na humfanya mtu huyo kuwa wazi kwa kile tunachokishiriki. Anaweza kupenya kizuizi chochote.

**Soma 1 Wakorintho 2:4-5**. Utakuwa na tofauti gani Mungu akikupa nguvu ya utendaji unapoanza kueleza imani

> **Mkristo aliyejazwa na Roho Mtakatifu kamwe hawezi kujikupata peke yake katika kushuhudia kwa moja kwa moja kwa sababu Yesu daima yu naye**

yako?

# 5

**Nafasi ya yesu**

Katika kumrejelea Yesu, Yohana mara kwa mara hutumia neno moja ambalol inaelezea nafasi yetu na Yesu.

Tazama Yohana 20:18, 25, 28; 21:7,15, 21, 24 Liandike neno hilo hapa.




Kujitambulisha na Yesu Kristo kwa maneno kama Bwana kutakupa msimamo imara unaposhiriki imani yako.

Marafiki zako wanapokuuliza ufanye jambo baya, wanapouliza ushauri wako, au wanapotaka tu kuzungumza, leta ubwana wa Kristo katika jibu lako.

Kwa mfano, rafiki anasema, "Twende tununue chupa sita za vileo Ijumaa usiku." Jibu lako la kawaida linaweza kuwa kama, "Mama yangu hataniruhusu." Lakini jibu bora zaidi ni, "Ninathamini mwaliko huo, lakini kwa sababu mimi ni mwana wa Yesu Kristo sitaki kufanya hivyo. Asante hata hivyo."

Rafiki yako katika darasa la Historia ananong'ona, "Hebu nioneshe jibu lako la swali la 12." Jibu lako la kawaida linaweza kuwa, "Vema, sistahili, lakini sawa." Badala yake unajibu, “Kwa sababu mimi ni wa Yesu Kristo, siwezi kukupa jibu. Lakini nitafurahi kukusaidia kusoma kwa mtihani unaofuata."

Maneno, “Kwa sababu mimi ni wa Yesu Kristo...” ni

maungamo ya kibinafsi kwamba Bwana Yesu anakumiliki. Pia ni kauli ya kijasiri kwa wengine. Wakati wowote uko chini ya shinikizo, kujaribiwa, au hofu. Sio tu kwamba yanakuweka katika nafasi ya kuepuka uchaguzi mbaya, lakini pia yanatoa ushahidi chanya kwa Yesu.

Wakati wa kwanza kuwataja wanafunzi, walikuwa wenye hofu na wamejifungia katika chumba – kujificha kutoka kwa mtu yeyote ambaye angeweza kufikiria kwamba walihusishwa na Yesu. Lakini wiki saba baadaye, walikuwa wameshinda hofu yao na walikuwa wakizungumza kwa ujasiri na watu kumhusu Yesu Kristo.




Sasa hivi unaweza kuhisi kama wanafunzi walivyohisi walipokuwa wameketi katika chumba kilichokuwa kimefungwa. Lakini Kristo aliyefufuka anaweza kukupa uwezo wa kuondoa hofu yako kama vile Yeye alivyowafanyia wafuasi Wake wa karne ya kwanza. Ili kufurahia uhuru kutokana na hofu na ujasiri wako katika kuwasilisha imani yako, chukua hatua hizi zifuatazo.

1. omba "sala hii ya hofu" ukimwomba Mungu ashinde roho ya hofu ndani mwako:

"Bwana Yesu, ninaleta hofu yangu mbele zako. Ninakiri

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Nataka Ubomoe kizuizi cha woga kinachonizuia kushiriki Imani yangu. Ninatamani maisha yangu yadhihirishe Roho Wako na nguvu Zako! Katika jina la Yesu Amina."

Omba maombi hayo kila siku hadi umalize kitabu hiki.

2. Shuleni tumia maneno: Kwa sababu mimi ni wa Yesu Kristo...
Tumia msemo huo kila mara unapoombwa kufanya

jambo lisilo la heshima kwa Kristo. Shirikiana na mtu katika kikundi chako ili kukusaidia kuanza.

**Kamilisha kipindi hiki kwa kukariri Warumi 3:23 na Warumi 6:23**.

## KAZI

1. kuwa na wakati peke yako na Mungu kila siku wiki hii, kwa kufuatia usomaji wa Biblia kutumia.

Siku ya 1: Matendo 4:1-12

Siku ya 2: Matendo 4:13-22

Siku ya 3: Matendo 4:23-37

Siku ya 4: Matendo 5:1-11

Siku ya 5: Matendo 5:12-26

Siku ya 6: Matendo 5:27-42

Siku ya 7: Matendo 6:1-15

2. Kamilisha Sehemu ya 3.

3. Kumbuka kuomba "sala ya hofu" na kutumia maneno, "Kwa sababu mimi ni mali ya Yesu Kristo…"

4. Pitia mistari uliyojifunza ulipojifunza *Kumfuata Yesu* hadi uinukuu kwa kikundi wiki ijayo.

# SEHEMU YA 3




# Ujasiri Katika Roho

Andy na Yohana huzungumza mara nyingi baada ya shule. Yohana ana mengi mazuri yanayomtendekea, lakini bado yeye anajitahidi kupata maana ya maisha. Andy anataka kumsaidia, lakini anahisi hivyo hatoshi...ni wa kawaida sana...hana nguvu.

Hisia za Andy ni za kawaida. Wengi wetu wanafikiri, mimi ni mtu wa kawaida tu...mimi ni nani nizungumze juu ya Yesu Kristo?

Unahisi kwa njia gani kuwa "mtu wa kawaida tu?"

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

Tuna mwelekeo wa kufikiria Wakristo wa Agano Jipya kama mashujaa wa ajabu na kuwa hawakuwa na udhaifu. Lakini walikuwa watu wa kawaida ambao walikuwa na matatizo kama hayo yetu. Ubora mmoja uliwatenga na kuwawezesha kuishi maisha kwa njia isiyo ya kawaida - walipitia kila siku uwezo wa ajabu wa Roho Mtakatifu.

**AHADI YA NGUVU**

Kabla ya Yesu kupaa mbinguni, aliwaambia wanafunzi wake waende katika nchi zote ulimwenguni na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi (Mathayo 28:18-20). Lakini Yeye alijua kuwa walihitaji nguvu zake kwa ajili ya kazi hiyo, kwa hiyo aliwaambia wasiondoke Yerusalemu mpaka walipojazwa nguvu za Roho Mtakatifu (Matendo 1:4).

**Kulingana na Matendo 1:8**, nini kinatokea kwa mtu “wakati Roho Mtakatifu anakuja?"

Matendo 1:8 ni ahadi ya Yesu ambayo inafungua mlango wa kueleza Imani yako kwa ujasiri. Inakuhakikishia uwezo wa kufanya mambo zaidi ya "kawaida." Lakini Yesu alitoa ahadi zaidi ya moja kuhusu Roho Mtakatifu.

Angalia mistari ifuatayo na uweke kila ahadi kwa maneno yako mwenyewe.

Yoeli 2:28

Marko 1:8

Luka 24:49

Matendo 1:5


Tambua kwamba unapokuwa na nguvu za Roho Mtakatifu, ushawishi wako unakuwa mkubwa zaidi na zaidi.

**Soma tena Matendo 1:8**. Tafuta kwenye ramani dunia ya Agano Jipya (Unaweza kuwa na moja nyuma ya Biblia yako.) Utapata

**Ahadi ya yesu ni kwamba Roho Mtakatifu atakufanya kuwa shahidi mwenye nguvu.**

kugundua

kwamba Yerusalemu ulikuwa mji ndani ya mkoa mdogo wa Yudea. Samaria ilikuwa sehemu ya kaskazini ya Yudea. (Wayahudi wengi waliwachukia Wasamaria.)
Na “miisho ya dunia” inajumuisha maeneo yote zaidi. Kwa hiyo Yesu alitaka wanafunzi wake waanzie pale walipokuwa, wasonge mbele,na hatimaye kuwafanya wanafunzi ulimwenguni kote..




Lakini maeneo ya kijeografia ambayo Yesu alitaja pia ni ishara ya maeneo yako binafsi ya huduma.

---‘’Yerusalemu" inawakilisha nyumbani kwako. Ni nani anahitaji ushuhuda wako nyumbani kwako?

---"Yudea" inaashiria marafiki zako. Ni yupi kati ya marafiki wako anayehitaji ushahidi wako?

--- "Samaria" inajumuisha adui zako na wale ambao ni wagumu Zaidi kuwapenda.
Ni adui yupi anayehitaji ushahidi wako?

---"Miisho ya dunia" inasimamia ushawishi wako unaowezekana
kubadilisha dunia nzima. Unadhani Mungu anaweza kukutumiaje
kusaidia kufikia ulimwengu?

Unapoanza kueleza imani yako kwa ujasiri kwa familia yako, marafiki zako, na adui zako, basi baada ya muda Mungu atakutumia kuuathiri ulimwengu mzima!

Nilikuwa na fursa ya kumwongoza mwanafunzi wa shule ya upili aitwaye Lee kwa Kristo. Mara moja akaenda nyumbani na kuwaambia wazazi wake kuhusu kuzaliwa kwake upya . Katika mwaka uliofuata alitumia nafasi yake kama mhariri wa gazeti
Kuchapisha kitabu cha mwaka cha shule kushiriki imani yake. Baadaye, akiwa kiongozi wa harakati za wakristo kwenye chuo chake, Lee alipata upinzani kwa imani yake kutoka kwa wasioamini. Lakini makala hasi za magazeti hazikumzuia. kwa sababu aliendelea kushiriki imani yake nyumbani kwake, na marafiki zake, na hata katika uso wa upinzani, Mungu aliheshimu ushuhuda wa Lee na ukaendelea. Baadaye, akawa mhariri wa gazeti lililomtangaza Yesu Kristo kwa wanafunzi wengi wa vyuo vikuu kuliko gazeti lolote duniani. Sasa, yeye ni mhariri wa jarida kubwa la kikristo duniani. Mwanzo ushuhuda wake ulianzia katika Yerusalemu, kisha kuhamia Uyahudi na Samaria, na sasa Mungu anamtumia Lee kufika miisho ya dunia kupitia ushuhuda wake kwa ajili ya Yesu Kristo.

**AHADI ILITIMIZWA**

Matendo 2 inaeleza kuja kwa Roho Mtakatifu. Wanafunzi walikuwa wakikutana pamoja wakati “wote walijazwa Roho Mtakatifu” ( Matendo 2:4 ) Kwa maneno yako mwenyewe, eleza tukio hilo ambalo limeelezwa kwa kina katika Matendo 2:1-4.

Mungu alitimiza nini kwa kuachilia nguvu za Roho Mtakatifu? ( Matendo 2:5-11 )

**Kila moja ya vifungu vifuatavyo** vinaeleza jinsi Roho Mtakatifu
aliwasaidia wanafunzi kuwasilisha imani yao. Andika unajifunza nini kutoka kwa kila kifungu:

Matendo 2:3

Matendo 4:8

Matendo 4:31

Matendo 6:1-6

Matendo 7:54-60.

Matendo 8:14-17

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

Matendo 9:17

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

Matendo 9:31

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

Matendo 10:44-48

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

Matendo 11:22-24

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

Matendo 16:6-10

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

Baada ya kuchunguza mambo yote ambayo Mungu alifanya katika maisha ya watu hawa wa kawaida kwa nguvu za Roho Mtakatifu, Hauoni ya kwamba anaweza kukupa uwezo wa kuongea na rafiki zako kumhusu Yesu?

> J.B. Phillips anaandika:
> Tofauti moja kubwa kati ya Ukristo wa siku hizi na ule ambao tunasoma ndani ya Biblia [barua za Agano Jipya] ni kwamba kwetu sisi kimsingi ni kama michezo ya kuigiza; kwao ilikuwa ni uzoefu wa kweli. Tunaweza kuyapunguza maadili ya Kikristo kuwa kama kanuni au bora zaidi, kanuni ya moyo na maisha. Kwa hawa wanaume ni wazi kabisa kwamba ulikuwa uvamizi wa maisha mapya kabisa. Hawakusita kuyaeleza haya kama Kristo akiishi ndani yao.
> (Barua kwa Makanisa Machanga, Macmillan)

Nguvu zile zile za karne ya kwanza -- nguvu za Roho Mtakatifu – zingali zinapatikana kwetu leo!

**NGUVU ILIYOFANYWA KUWA YA KIBINAFSI**

Yesu anataka tujazwe na Roho Mtakatifu ili tuweze kuishi kwa kuwaambia wengine juu yake.

Tulijadili jinsi ya kujazwa na Roho Mtakatifu katika Sehemu ya 7, katika kitabu cha *Kufanya Yesu Kuwa Bwana*. Kagua sura hiyo na ufanye muhtasari wa kile unachogundua.

____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________

---Kumbuka kuombea ujazo wa Roho Mtakatifu kila siku.
---Andika maombi ya kumwomba Roho Mtakatifu akujaze ili uweze kuwa na uwezo wa kushuhudia Kristo.

____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________

**Soma Wagalatia 5:22-23**. Sasa chunguza matokeo ya kuwa na
nguvu za Roho Mtakatifu ndani yako. Una sifa gani wakati "umejazwa na Roho Mtakatifu?"

____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________

**Soma 1 Wathesalonike 1:5**. Eleza jinsi Roho Mtakatifu anaupa ujumbe wako nguvu ya ajabu.

____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________

Kuwasiliana kumuhusu Yesu si rahisi. Nikiwa katika chuo nilijaribu kuongea na Craig juu ya Yesu. Lakini nilimkasirisha kwa kumsukuma kwa nguvu sana na hoja

zangu binafsi bila kujali. Matokeo yake, alianza kukikwepa chumba changu na hatukuzungumza tena juu ya Kristo.

Baadaye, nilipokuwa nikicheza mpira wa vikapu na timu ya *Athletes In Action*, kiongozi wa timu yetu alinieleza jinsi ningeweza kujazwa na Roho Mtakatifu. Hiyo ilileta Mabadiliko mapya katika maisha yangu ya kiroho. Nilianza kupata ujasiri mpya, huruma, na usikivu ambao sikuwa nao hapo awali.

Siku moja mchana, siku chache baadaye, mimi na rafiki yangu tulipata fursa tatu za kuzungumza na wanariadha kutoka Chuo Kikuu cha Northern Illinois. Tulitumia mchana wote kuzungumza, kusikiliza, na kushiriki Injili. Watu hao wote watatu walimpokea Kristo.

Tofauti ya matukio hayo mawili ilikuwa ni Roho Mtakatifu..

**KUSHUHUDIA KATIKA ROHO**

> **Wakati sisi Tunajazwa na Roho Mtakatifu, tunayo nguvu ya kumshiriki Kristo.**

Baada ya wanafunzi kupata nguvu wa Roho Mtakatifu, wakaanza kuzungumza juu yake Yesu Kristo. Katika Matendo 4 (baada ya kumponya kiwete) Petro na Yohana, watu wa kawaida, walionyesha dalili tano za ushuhuda katika nguvu isiyo ya kawaida ya Roho Mtakatifu. Ishara hizo tano zitakuwepo wakati tunashuhudia kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Hebu tuzichunguze.

**1 Mateso** Katika Matendo 4:18-21, Petro na Yohana waliletwa mbele ya Sanhedrini. Kwa nini?

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

Petro anatuambia kuwa ni jambo la heshima kuteseka kwa ajili ya Kristo.

> **Wakati sisi tutashuhudia katika nguvu za Roho Mtakatifu, mateso yatatufuata..**

**Kutoka kwa maandishi ya Petro katika 1 Petro 4:12-16**
inaeleza jinsi unaweza kuteswa kwa ajili ya kumshiriki Kristo.

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

Mtu ameuliza swali: "Ikiwa ungekamatwa kama mfuasi wa Yesu Kristo, Je, kungekuwa na ushahidi wa kutosha kukuhukumu?"
Katika kesi ya Petro na Yohana, jibu lilikuwa ni wazi. Ndiyo. Je, kutakuwa na ushahidi wa kutosha wa kukutia hatiani? .

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

## 2 Kuelekeza kwa Yesu

Petro na Yohana walielekeza watu kwa Yesu. Walikuwa wamesadikishwa kabisa kwamba njia pekee ya kumjua Mungu ilikuwa kupitia kwa Yesu Kristo.

**Soma Matendo 4:8-12** na uandike baadhi ya mambo waliyokuwa wakiyafanya ili kuwaelekeza wengine kwa Yesu.

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

Unaweza kujifunza nini kutokana na uzoefu wa wanafunzi ili kukusaidia kuwaelekeza rafiki zako shuleni kwa Yesu?

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

## 3 Ujasiri

Petro na Yohana walizungumza kwa ujasiri. Hawakuwa na hofu au kutishwa na watu waliokuwa karibu nao.

**Soma Matendo 4:13**. Ujasiri wao ulishinda kikwazo gani?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Fikiria fursa ya kuonyesha ujasiri shuleni, unaweza kuonyesha vipi ujasiri katika hali hiyo?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

## 4 Maisha Yaliyobadilishwa

Viongozi wa kidini walitambua kwamba Yesu Kristo alikuwa na mvuto mkubwa sana kwa Petro na Yohana.

**Soma tena Matendo 4:13.**

Je, marafiki zako wanaweza kuona mvuto mkubwa wa mabadiliko ndani yako? Kwa njia zipi?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

## 5 Sifa kwa Mungu

Petro na Yohana hawakuwa pekee waliokuwa na maisha yaliyobadilika. Hapanamtu angeweza kukana kwamba yule kilema alikuwa ameponywa, kwani alikuwa ameponywa na amesimama pamoja nao (Matendo 4:14). Tena hakuna mtu ambaye angedai kuwa wanafunzi walikuwa na uwezo wa kuufanya muujiza huo. Maisha yaliyobadilika ya mtu huyu kilema yangeweza tu kuhesabiwa kwa uwezo wa Mungu pekee. Licha ya ukweli kwamba matukio haya yasiyo ya kawaida yalifanyika kupitia kwa Petro na Yohana, wao walikuwa wepesi wa kumpa Mungu sifa.
**Kutokana na Matendo 4:21-22**, matokeo ya wao kueleza imani yao yalikuwa nini?

______________________________________________
______________________________________________

________________________________________________
________________________________________________

Je, haifurahishi kujua hayo unaposhuhudia kwa nguvu za Roho Mtakatifu, matokeo yatakuwa kwamba watu wengi watamsifu Mungu? Shuleni kwako, watu wengi wanataka kumjua Yesu na wakristo wengi wanataka kushuhudia. Mfano wako wa kushuhudia unaweza kuanzisha wimbi moja la wasio wakristo kuja kumjua Kristo na wimbi jingine la Wakristo ambao, kupitia kushuhudia kwako watapata ujasiri wa kushuhudia kwa ajili ya Kristo.

Fikiria nyuma katika maisha yako na uorodheshe kila mtu ambaye ushahidi wake uliathiri uamuzi wako wa kuwa mfuasi wa Yesu. Msifu Mungu kwa kila mtu kwenye orodha yako.

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

Sasa orodhesha baadhi ya watu wanaoweza kumsifu Mungu kwa sababu ya ushuhuda wako kwao.

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

Kushuhudia kwa kawaida hakuleti matokeo ya haraka. Hakuna dhamana au fomula za kifumba macho. Lakini unaposhuhudia kwa uaminifu, basi Mungu ataleta matokeo kwa uaminifu kwa wakati ufaao.
Punde tu baada ya kuwa mwamini, ilinibidi kutoa hotuba ya ushawishi katika darasa langu la hotuba. Niliamua kuzungumzia jinsi nilivyomjua Kristo. Nilitaka kulishawishi darasa kufanya vivyo hivyo. Nilisoma kwa bidii ili kujiandaa kwa hotuba. Niliiwasilisha ujumbe kwa ujasiri. Lakini profesa na wanafunzi wenzangu walipoitathmini hotuba yangu waliikataa katakata.

Tulipotoka darasani, mwanafunzi mwenzangu alisema, "St. Clair, wewe kweli umejitengenezea uzuzu mara hii." Niliporudi chumbani kwangu, jamani ujasiri wangu ulikuwa umetoweka kabisa.

Lakini miaka minne baadaye, dada yangu alikutana na rafiki anayeitwa Clay. Aligundua kwamba amekuwa kiongozi wa Kikristo, na alikuwa ameandika kitabu hivi karibuni kuhusu jinsi  Kristo alivyoYAbadilisha maisha yake. Alimuuliza jinsi alivyokuja kumjua Kristo.  Akajibu, "Katika darasa la hotuba chuoni, kaka yako Barry alitoa hotuba jinsi Kristo alivyobadilisha maish yake. Hotuba yake ilinifanya nifikirie, na mimi nikamkubali Kristo."

Ilinichukua miaka minne kutambua kwamba hotuba yangu ilikuwa na matokeo mema. Hili tukio moja linatukumbusha kwamba tunahitaji kushiriki imani yetu kwa ujasiri na katika nguvu za Roho Mtakatifu na kumwachia Mungu matokeo..

**Mshiriki Kristo katika**
**Nguvu za Roho Mtakatifu**
**na umuachie Mungu matokeo**




**Kutana** wiki hii na mtu mwingine katika kikundi chako. Chagua rafiki ambaye si muumini ambaye unaweza kujadili mahusiano yako na Kristo pamoja naye. Kumbuka kwamba nyinyi ni watu wa kawaida wenye nguvu isiyo ya kawaida. Mungu atakutumia zaidi ya uwezo wako. Kisha…

1.mwombee rafiki ambaye utamshuhudia.
2. Weka muda wa kukutana na rafiki yako.
3. Zungumza na mtu huyo kwa ujasiri kuhusu kile ambacho Yesu Kristo anamaanisha kwako.

**Kamilisha kipindi hiki kwa kukariri Waebrania 9:27.**

# KAZI

1. Endelea na nyakati zako za kila siku peke yako na Mungu, ukitumia kufuatia usomaji wa Biblia.

Siku ya 1: Matendo 7:1-16

Siku ya 2: Matendo 7:17-34

Siku ya 3: Matendo 7:35-53

Siku ya 4: Matendo 7:54-8:3

Siku ya 5: Matendo 8:4-25

Siku ya 6: Matendo 8:26-40

Siku ya 7: Matendo 9:1 -19a

**2. Kamilisha sehemu ya 4.**

3. tekeleza mradi wako wa kuzungumza na rafiki asiye mwamini wakati Fulani wiki hii.

4. Rudia mistari mitano ya kwanza ya kumbukumbu kutoka kwa *Kutumia Wakati Peke Yako na Mungu* kunukuu kwa kikundi wiki ijayo.

# SEHEMU YA 4




## Kuwafanya Marafiki Wa Kristo

Andy na Yohana wamekuwa marafiki. Shule ilipoanza mwaka huu, wao hawakujuana hata kidogo. Walichokuwa nacho kwa pamoja ni darasa la Kiingereza. Lakini mahali Fulani, urafiki ulianza.

Pengine hakuna rafiki wawili wanaofanana kabisa, lakini wote wana baadhi ya vipengele vya kawaida vinavyofanana. Fikiria urafiki mmoja ulio nao sasa. Urafiki huo ulianza vipi? Ulifanya nini ili kuendeleza?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

HURUMA - KIUNGO CHA MSINGI

Urafiki mara nyingi huchukuliwa kuwa wa kawaida. Watu wengine hufikiri, "Ninao marafiki wote ninaowahitaji." Lakini wanakosea. Watu wengine wanawahitaji!
Yesu anataka tuwe marafiki na watu wengi kadiri tuwezavyo. Inatubidi tuwatafute watu wanaohitaji marafiki na tujitolee kwao.

**Soma Mathayo 9:35–38** na uandike chini ya umaizi wako kuhusu jinsi Yesu anataka tuwatendee watu wengine.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Tunaambiwa kwamba Yesu alikuwa na huruma. Angalia ufafanuzi wa neon huruma na uandike hapa chini.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

**Soma ufafanuzi wa Paulo wa neno huruma katika 1 Wakorintho 1 3** . Anatumia neno la Kigiriki agape, ambalo limetafsiriwa kama "upendo." Upendo wa Agape hauna masharti.

Ni Mungu pekee anayependa bila masharti. Tunapata uzoefu huu wa upendo usio na masharti kwa kumjua Yesu Kristo. Na tunaweza kupenda bila masharti tu kwa

kumruhusu Roho Mtakatifu kuwapenda wengine kupitia kwetu.

Tunaitikiaje upendo wa Mungu wa agape? Kwa kumpenda na kumtii. Kupitia upendo na utii wetu, Mungu atajaza huruma kwa wengine katika maisha yetu. Upendo wa Mungu wa agape huwa ndani yetu kila wakati, hata wakati hatufanyi kuueleza hivyo. Mungu anataka tuimwage - sio matone tu hapa na pale, lakini ikimwagika kama glasi chini ya bomba lililo wazi. Jinsi tunavyomwaga, ndivyo Mungu atakavyozidi kutujaza.

Mungu hajalishwi kama wewe ndiye mdadisi mkuu katika shule yako, mchezaji bora wa kandanda au mshangiliaji, mwanamuziki mkuu zaidi, au rais wa kundi lako la vijana. Vipaji vyako vyote havimjalishi kama huwapendi watu wengine.

**Soma 1 Wakorintho 13** tena na uandike orodha ya vitu ambavyo si upendo. Baada ya kila kitu unachoorodhesha, uliza kwa uaminifu, Je! katika maisha yangu, vitu hivi vimo maishani mwangu? Andika chini mifano yoyote maalum ambapo haya yameonekana katika maisha yako. Kisha mwombe Mungu azibadilishe tabia hizo na upendo Wake.

| **Upendo si** | **Jinsi ninavyoonyesha tabia hii** |
|---|---|
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |

Tunapokutana na watu waliopotea bila upendo hakuna matokeo mema.

Mungu anataka tuachane na tabia zinazotuzuia tusiwapende wengine. Muulize aanze kukuondolea tabia mbaya kwa...

--- Kufichua jinsi ambavyo kikweli huna upendo;
--- Kuondoa mitazamo yako yote mibaya, kwa kutumia njia yoyote muhimu;
- Kubadilisha mitazamo yako isiyo na upendo na huruma.

**Sasa soma 1 Wakorintho 13** kwa mara nyingine tena. Na wakati huu tengeneza muhtasari wa mapenzi ni...

| **Upendo ni** | **Jinsi ninavyoonyesha tabia hii** |
|---|---|
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |
| ____________ | ______________________________________ |

Tunaporuhusu upendo wa Yesu kutiririka ndani yetu, watu wengine huwa wazi Zaidi kusikia tunachosema.

**Soma 1 Wakorintho 13 mara tena**, kama unataka kufanya
Upendo wa Mungu kuwa wa kibinafsi zaidi. Sasa badilisha kila neon kuhusu "upendo" na neno "Yesu." Kwa mfano: Yesu ni mvumilivu...Yesu ni mwema...

Kwa kuwa Yesu anaishi ndani yetu, tayari ameweka sifa hizo za upendo ndani mwetu sisi. Lakini bado lazima tujifunze kumwamini Yeye kila siku ili kuzieleza sifa hizo kupitia kwetu.

**KWANINI UWE RAFIKI?**

Yesu aliwaona wasioamini kuwa "walionyanyaswa na wasiojiweza, kama kondoo wasio na mchungaji".

**Katika Mathayo 9:36** walikuwa wamepotea, wakitanga-tanga, wasijue walikokuwa wakienda, bila marafiki wa kweli wa kuwaongoza. Labda una marafiki katika hali kama hii ambao wanahitaji kumjua Yesu Kristo.

Je, kwanini marafiki zako wasio Wakristo wanahitaji urafiki wako sana?
Fikiria sababu zifuatazo.

**1 Marafiki Ni Wafariji**
Je, unaweza kufikiria mtu ambaye ana matatizo lakini hanamarafiki wa kushiriki nao matatizo hayo? Unafikiri mtu huyo anahisije?

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

Marafiki huwafariji wengine: “Afadhali kuwa wawili kuliko mmoja, kwa kuwa wana faida nzuri kwa kazi yao: Mtu akianguka chini, rafiki huyu anaweza kumsaidia kuinuka.
Lakini mhurumieni mtu anayeanguka na hana mtu wa kumsimamisha!” (Mhubiri 4:9-10).

Wazia juu ya mistari hii na ufikirie baadhi ya njia unazoweza kuwafariji marafiki zako wasio Wakristo.

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

**2 Marafiki Ni Washauri**
Unajua watu ambao wanaelekea kwenye njia mbaya. Kama nyinyi ni marafiki, mtu huyo angesikiliza ushauri wako. Kuwa rafiki wa mtu hukupa fursa ya kusikiliza matatizo na
kisha kutoa ushauri.

Biblia inahimiza aina hiyo ya uwazi na uaminifu kati ya marafiki. "Karipio la wazi ni bora kuliko upendo uliositirika" (Mithali 27:5). Hiyo inakufanya kuwa mshauri kwa rafiki yako.
Je, ni baadhi ya njia gani unaweza kumsaidia rafiki yako kwa tatizo lake?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Unawezaje kusaidia kumfanya rafiki yako awe karibu na Mungu?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Marafiki Hupeana Changamoto
Wengi wetu tunajua watu ambao wanahitaji kuanza kujishughulisha kama watafikia uwezo wao kamili. Wanahitaji kusoma, kufanya mazoezi, kutumia muda wao vyema, au kupata motisha. Marafiki wa kweli huwapa changamoto kwa kila mmoja katika kila nyanja ya maisha yao. Biblia inahimiza ili tunoane sisi kwa sisi. "Kama vile chuma hunoa chuma, ndivyo mtu mmoja amunoavyo mwingine" (Mithali 27:17).

Ni kwa njia gani unaweza kuwa mtia changa ambaye "humnoa" rafiki yako asiye Mkristo?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

**KUFANYA MARAFIKI**

Mojawapo ya urafiki wa karibu sana katika historia ulikuwa kati ya Daudi na Yonathani ( 1 Samweli 18:1-4 ). Urafiki huo unaweza kutusaidia kuimarisha urafiki wetu pamoja nao watu wasiomjua Kristo.

Inashangaza kwamba Daudi na Yonathani walikuwa marafiki – wacha hata kuwa marafiki kidogo tu! Yonathani alikuwa mwana wa Mfalme Sauli, na kwa haki zote alipaswa kuwa katika mstari wa kuurithi ufalme. Lakini Mungu alikuwa amemteua Daudi kama mrithi wa Sauli. Daudi alijulikana sana kwa ujasiri wake, kwanza kama mchungaji na pia kama muuaji wa Goliathi.

Yonathani alikuwa shujaa mkuu aliyewaua maelfu ya Wafilisti. Yeye alikuwa jasiri. Yeye na mbeba silaha wake waliwaua watu 20 kwa wakati mmoja (I Samweli 14:14). Watu walimpenda. Kwa hiyo fikiria jinsi angeweza kuhisi alipogundua kwamba Daudi, ndiye angekuwa mfalme anayefuata na wala si yeye mwenyewe,.

Wacha tuweke hali hii vingine ili kuileta karibu nawe.

--- Fikiria umekuwa mshangiliaji mkuu wa timu yako tangu darasa la saba. Kabla ya timu kuingia katika michuano ya kujaribu, msichana mpya anahamia mjini, na kukushinda
na kuwa kiongozi mkuu badala yako.

---Fikiria umekuwa ukicheza mpira wa vikapu tangu ulipokuwa kijana wa kutosha kupiga chenga. Unajitayarisha kuanza mwaka wako wa juu darasa la juu wakati mwanafunzi wa urefu wa 6' 10" anapohamia shuleni kwako na kukutimua
kutoka kwa timu ya kwanza.

---Fikiria kuwa unachumbiana na msichana unayemjali sana. Lakini yeye anaamua kuwa anampenda rafiki yako bora zaidi, na wawili hao wanaanza kuchumbiana.

Katika hali kama hizi, unaweza kudhihirisha zaidi tabia za upendo usivyo kuliko tabia za "upendo ni nini." Ni vigumu kuwa mwenye subira na fadhili wakati matumaini yako yanapovunjwa. Hata hivyo tazama Yonathani na jinsi alivyoitikia kwa upendo kwa mtu ambaye alikuwa na uwezo wa kuwa adui yake, Daudi. Hata kama hatuvutiwi kiasili na watu ambao ni vigumu kuwapenda, Mungu anawapenda
wao. Anataka kuwafanya marafiki zake. Anafanya hivyo kwa kututumia sisi kuwafanya marafiki zetu

**Mungu anawapenda watu ambao sisi tunapata ugumu kuwapenda.**

**Angalia 1 Samweli 18:1-4** na utafute hatua nne ambazo Yonathani alizichukua ili kusitawisha urafiki mkubwa pamoja na mtu ambaye angeweza kuwa adui yake, Daudi.

**1 Kivutio**
"Yonathani akawa katika roho mmoja na Daudi" (1 Samweli 18:1). Jonathan alichukua hatua ya kwanza kujenga urafiki huo. Ikiwa unayo shida kuanzisha mazungumzo na urafiki, tumia mapendekezo yafuatayo.
---" Sema "*Habari."* Badala ya kutembea kwenye ukumbi kichwa chini, jifunze kutabasamu na kuwa na urafiki.
Haiwezi kuwa kwa bahati kwamba mtu anaipita njia yako. Mungu anaweza kutaka wewe, kwa njia fulani, kuyaathiri maisha ya mtu huyo. Kwa kusema "Habari" kwa tabasamu, unaweza kufungua njia ya kuanza uhusiano.

--- *Kumbuka majina*. Ikiwa hujui jina la mtu, uliza. Baada ya
kuuliza, kumbuka. Tumia hilo jina mara kadhaa ili kuhakikisha kwamba unalikumbuka. "Habari, Yohana, mambo vipi, Yohana?

--- *Kuuliza maswali*. Wakati huwezi kufikiria chochote cha kuzungumza, Jifunze kuendeleza mazungumzo kwa kuuliza maswali tu katika kila eneo. Kwa mfano,"Unamjua Fred? Je! unacheza nafasi gani katika soka? Ulipataje kupendezwa nayo? Nini somo unalolipenda zaidi? Usilolipenda? Kwa nini? Nini mapambano yako makubwa? Unafikiri wakati ujao utakuwa na nini kwako?"

--*Waziingatie kikamilifu*. Waangalie machoni. Usiangalie kandokando na kujifanya kama kwamba hupendezwi. Kuwasikiza wengine sio jambo la moja kwa moja. Inagharimu mazoezi.

Ni watu gani watatu ungependa kuwaambia "Habari" au kuendeleza mazungumzo nao wiki hii? Andika majina yao kwenye nafasi ifuatayo.

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

## 2 Mapenzi

“Na [Jonathani] akampenda [Daudi] kama nafsi yake (1 Samweli 18:1) Daudi na Yonathani walisitawisha ukaribu sana hivi kwamba Yonathani alisaidia kumulinda Daudi kutoka kwa baba yake mwenyewe, Sauli.

Unawezaje kuendeleza mapenzi kwa watu wengine - hasa wale ambao si waumini?

---Gundua malengo ya pamoja. Inaweza kuwa mpira wa vikapu au jambo linguine lolote. Kama ukiangalia utapata kitu ambacho mnafanana kwacho.
--- Jenga uzoefu wa makubaliano kuelekea malengo hayo. Fanya jambo hilo linalokuwezesha kufikia malengo yako pamoja.

Kwa kila mmoja wa watu watatu ulioorodhesha, andika lengo moja la pamoja na uzoefu unaoshiriki na mtu huyo.

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

## 3 Uwajibikaji

Yonathani alifanya agano na Daudi (1 Samweli 18:3). Walikuwa wakijitolea kwa kila mmoja. Kufanya maagano katika Agano la Kale lilikuwa ni jambo kubwa. Ilikuwa haiwezi kuvunjika. Katika agano, watu walitoa kila mmoja zawadi ya thamani kubwa. Zawadi hiyo ilionyesha kujitolea na uwajibikaji. Urafiki wa agano hakika ulikuwa wa kina-kuliko uhusiano wa kawaida

Unawezaje kusitawisha urafiki wa kina zaidi? Na marafiki zako wanaoamini? Na rafiki asiye Mkristo? Gundua mahitaji na matamanio ya marafiki zako. Wasaidie kutimiza mahitaji na matamanio yao. Mruhusu rafiki yako kugundua na kutimiza mahitaji na matamanio yako.

Kwa kila mmoja wa watu watatu ulioorodhesha hapo awali, andika njia moja maalum ambayo unaweza kuimarisha urafiki huo.

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

**4 Upendo wa agape**
Yonathani akavua vazi alilokuwa amevaa, akampa Daudi; pamoja na vazi lake, na hata upanga wake, na upinde wake, na mshipi wake." (I Samweli 18:4). Hizi zilikuwa ishara ya utayari wa Yonathani kufanya dhabihu za kibinafsi kwa ajili ya Daudi. Ndivyo ilivyokuwa kwa Daudi kumuelekea Yonathani. Walikua katika urafiki wao hadi ikafikia kiwango ambapo wao walikuwa tayari kufa kwa ajili ya kila mmoja wao.

Yesu akasema, Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa rafiki zake." ( Yohana 15:13 ) Unawezaje kufikia kiwango hicho cha urafiki?

---Pitia furaha na maumivu pamoja.
---Shiriki nguvu na udhaifu wao.
---Tatua migogoro inapotokea kwa kujifunza kuomba msamaha.

Fikiria watu hao watatu kwenye orodha yako kwa mara nyingine tena. Amua njia moja ya vitendo ambayo unaweza kujitolea kibinafsi kwa kila mmoja wa marafiki zako.

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

**SHUGHULIKIA KWA MAOMBI**

Hitaji kuu la marafiki wasio Wakristo ni kumjua Yesu Kristo. Wewe jaza hitaji hilo kwa kuwaombea na kwa kushiriki habari njema ya Kristo nao. Maombi yako thabiti yatasaidia kuvunja upinzani wa marafiki zako wasioamini kwa Kristo.

Hivi ndivyo unavyoweza kutengeneza mkakati wa maombi.

Kutana na marafiki wawili kutoka kwa kikundi chako cha uanafunzi au kikundi cha vijana na omba pamoja mara kwa mara kwa ajili ya marafiki zako ambao hawajamjua Kristo. Uwepo wa Mungu utakuwa pamoja nawe. Yesu aliahidi, “Walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa jina langu, hapo nipo pamoja nao” (Mathayo 18:20).

KUTANA { NA WAKRISTO WA / MARA / NA WATU WA } 3 KWA JUMA KUOMBA KWA AJILI YA WATU WASIO WAKRISTO

**Andika majina ya washirika wako wa maombi ya Kikristo hapa.**

1. Jina lako ______________________________
2 . ______________________________
3 . ______________________________

**Andika majina ya marafiki zako wasioamini hapa.**

1 . ______________________________
2 . ______________________________
3 . ______________________________

**Amua lini mtasali pamoja na iandike hapa:**

1 . ______________________________
2 . ______________________________
3 . ______________________________

**HAPA PANA USAIDIZI**

Unaweza kugundua jinsi ya kufanya hivyo kwa undani kwa kuangalia Njia Ya Ajabu Ya Kuomba katika www.reach-out.org au piga 1.800.473.9456.

Unapomuombea rafiki asiye Mkristo, tambua kuwa pale msalabani Yesu tayari amemnunua mtu huyo kama mali yake mwenyewe. Kwa sababu hiyo unaweza kuomba...

---Kwamba Mungu atabomoa ngome zinazowaweka marafiki zako kutompokea Kristo (2 Wakorintho 10:4-5).

---kwamba marafiki zako watatubu na kuamini.

---Ili kusudi la Mungu litimie ndani yako na kupitia kwako maisha ya marafiki.

Kupitia maombi, unaweza kuwasilisha marafiki zako kwa Mungu. Unapowaombea marafiki zako, Mungu atafanya kazi katika maisha yao kuwaleta kwake.

> **Unapowaombea marafiki zako, Mungu atafanya kazi ndani yamaisha yao ili kuwaleta kwake.**




**Amua** marafiki watatu wasio Wakristo ambao utazingatia maombi yako kwao. Tengeneza orodha ya kila mtu ambaye ungependa kuona akimjua Kristo (jamaa, wanafunzi wenzako, au watu kazini kwako.) Kisha amua wale ambao unawapa vipaumbele ili kuwafikia kwa ajili ya Kristo. Mwambie Bwana aseme nawe. Unapoomba, zingatia chaguzi hizi:

--- Wale unaofikiri wako karibu zaidi kumjia Kristo.

---Wale ambao unakuwa nao mara kwa mara na mawasiliano mazuri.

---Wale ambao wameonyesha kupendezwa kiroho.

---Wale wanaokuheshimu.

---Wale ambao unaweza kuwa na muda mdogo wa kuwafikia.

---Wale ambao Roho Mtakatifu amekupa wewe kuwawajibikia kiroho.

---Wale ambao Mungu anaonekana kuwaleta kwenye njia yako mara kwa mara.

2.Tengeneza orodha ya mwisho ya watu watatu unaowapa vipaumbele vyako vya juu zaidi. Andika majina yao hapa:

_____________________________________________
_____________________________________________
_____________________________________________

3. Ombea marafiki hawa watatu kila siku.

4. Kutana na marafiki zako Wakristo mara kwa mara kuwaombea marafiki wasio Wakristo.

5. chukua hatua moja hususa kuonyesha urafiki wako kwa kila mmoja wa hao marafiki watatu wasioamini.

_____________________________________________
_____________________________________________
_____________________________________________

**Kamilisha kipindi hiki kwa kukariri Warumi 5:8.**

## KAZI

1. Endelea na nyakati zako peke yako na Mungu wiki hii, ukitumia usomaji wa Biblia ufuatao:

   Siku ya 1: Matendo 9:19b-3l

   Siku ya 2: Matendo 9:32-43

   Siku ya 3: Matendo 10:1-16

   Siku ya 4: Matendo 10:17-33

   Siku ya 5: Matendo 10:34-48

   Siku ya 6: Matendo 11:1-18

   Siku ya 7: Matendo 11:19-30

   **2. Kamilisha Sehemu ya 5.**

   3. Fuatilia maombi yako na matendo ya urafiki kwa makafiri wako wasioamini.
   4. Pitia mistari yote ya kumbukumbu uliyojifunza ulipojifunza *Kumfuata Yesu*, *Kutumia Muda Peke Yako na Mungu*, na *Kumfanya Yesu kuwa Bwana*..

# SEHEMU YA 5




## Kuanzisha Mazungumzo

Kila siku kwa wiki iliyopita Andy amekuwa akimuombea Yohana na kumuuliza Mungu amufungulie nafasi ya kuzungumza juu ya Yesu Kristo. Leo, wapo wanakwenda nyumbani baada ya shule. Andy anahisi kuwa hii ndiyo fursa aliyonayo aliokuwa akiisubiri, lakini hajui jinsi ya kuanza. Anawezaje kumuleta Kristo kwenye mazungumzo?

Andika mapendekezo machache unayoweza kumpa Andy.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Ikiwa una wasiwasi kuhusu jinsi ya kuanza mazungumzo kuhusu Yesu Kristo, jiunge nami. Simjui mtu yeyote ambaye hana ugumu wa kuanza katika mazungumzo. Hata hivyo kunao wengine ambao wamejifunza kuzungumza juu ya Yesu Kristo na unaweza pia kuwa kama wao.

MFANO BORA ZAIDI
Ikiwa unaamua kuwa mwanariadha mzuri, mwanamuziki, au mwanafunzi, njia bora Zaidi kuanza ni kumtafuta mwanamitindo. Tafuta mtu anayefaulu katika eneo hilo na gundua jinsi mtu huyo alivyofanya akafaulu. Mfano bora wa kujifunza jinsi ya kuishiriki imani yako ni Yesu Kristo Mwenyewe, kwa hivyo tuangalie na tujifunze kutoka kwake Yeye.

**Soma Yohana 4:1-42**, ambayo inaelezea kukutana kwa Yesu
pamoja na mwanamke Msamaria. Unaposoma kifungu hiki, andika
baadhi ya vizuizi ambavyo Yesu alikumbana navyo na jinsi alivyovishinda.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

**VIVUNJA VIZUIZI**

Kulingana na kukutana kwa Yesu na yule mwanamke kisimani, acha tuangalie baadhi ya njia alizozitumia ili kuvunja vizuizi ili kuwezesha mazungumzo kuelekea mambo ya kiroho. Unaweza kutumia vivunja vizuizi vyako vile vile.

**1 Tulia**
Yesu alikuwa ameketi kisimani - amechoka, bila mpangilio, na amestarehe. Ni kawaida kuingiwa baridi wakati somo la Yesu linapotokea, lakini mkazo huu utatoweka ikiwa utapumzika tu na kujirejelea mwenyewe. Usijisikie kama wewe inakubidi kulazimisha mazungumzo. Mungu anataka kukutumia kueneza ujumbe Wake, lakini ni juu ya Roho Mtakatifu

kumbadilisha rafiki yako. Ikiwa unayo mikono ya wasiwasi, mabega yenye mkazo, na sauti ya kufinya wakati wa mazungumzo, yaelekea utaona kushindwa hata kabla ya kuanza kuzungumzia mambo ya kiroho. Vibaya zaidi, utamfanya rafiki yako ahisi wasiwasi.

Andika mawazo yako juu ya unavyoweza kutulia, kuwa wewe mwenyewe, na kumfurahia rafiki yako.

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

## 2 Uliza Maswali

Yule mwanamke alipokuja kuteka maji, Yesu akauliza, "Je, utanipa maji?" Hii ilikuwa njia nzuri ya kuanza mazungumzo. Ikiwa una wasiwasi kuhusu neno la kusema na jinsi ya kuendelea na mazungumzo, kumbuka tu kuuliza maswali. Na ikiwa unakuja kwa mtu ambaye jibu lake pekee ni ndiyo au hapana, uliza maswali yanayoanza na Nani? Nini? Wapi? Lini? na Kwanini? Maswali haya yatakusaidia kumleta rafiki yako kwenye mazungumzo.

Andika maswali ambayo unaweza kumuuliza rafiki yako.

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

## 3 Sikiliza

Yesu alimsikiliza kwa makini mwanamke huyo. Alisikiliza vya kutosha, hakusikiliza tu kile alichokuwa akisema, bali pia kile ambacho hakuwa akisema. Tunahitaji kujifunza jinsi ya kusikiliza kwa hisia sawa.

Unaonyesha kupendezwa na mtu mwingine unapomsikiliza, badala ya kukatiza au kulazimisha maoni yako mwenyewe. Sikiliza kwa subira kwa mahitaji, hofu, matatizo na maswali. Jinsi utakavyomuelewa mtu mwingine, ndivyo unavyopata nafasi nzuri ya kuzungumza naye juu ya Kristo.

Je, unasikiliza vizuri? Orodhesha mielekeo yako chanya na hasi katika kuwasikiliza wengine.

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
_____________________________________________

**4 Chunguza Maslahi ya pamoja**
Yesu alimwambia mwanamke Msamaria kwamba ana kiu. Ni wazi, mwanamke alikuwa amekuja kisimani kutafuta maji. Yesu aliweza kuanza mazungumzo kulingana na maslahi yao ya kawaida katika maji.

Unajitambulisha vipi na marafiki zako? Kupitia michezo? Muziki? Kazi ya nyumbani? .marafiki wa kawaida? Andika baadhi ya masilahi ya kawaida uliyo nayo na marafiki wako wasioamini.

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

**5 Tafuta Kiini**
Yesu alimwambia mwanamke amchukue mumewe na arudi. Alisema, yeye hakuwa na mume. Yesu alikubali, lakini akamwambia alikuwa nao hapo awali waume watano na kwa sasa alikuwa akiishi na mwanamume ambaye hakuwa mume wake. Hakika Yesu aligusa kwenye mshipa wake!

Je! unakumbuka kuumwa kwako kwa meno mara ya kwanza? Kama daktari wa meno alivyokuchunguza, hakuna kitu kilitokea mwanzoni alipokuwa akikukagua. Lakini alipofika kwenye jino lililokuwa likigonjeka, aluguza mshipa na ukahisi kuruka juu kwa uchungu.

Marafiki wako wana mishipa nyororo pia. Kama unaweza kugundua nini upi, utakuwa na usikivu wao kamili. Hapa kuna Zaidi ya "neva" nyeti za kawaida

ambazo marafiki wako wanaweza kuwa nazo.

- wazazi
- picha ya kibinafsi
.- uaminifu
-uchumba/ngono
-mpenzi/mpenzi
- alama
-marafiki/upweke
- kujiua

Kumbuka, hii ni mishipa nyororo. Kadiri unavyozidi kuwa laini, ndivyo inauma zaidi mtu akiigusa. Kuwa makini.

Unadhani ni mishipa gani iliyo wazi Zaidi katika kila mmoja wa marafiki zako wasioamini?

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

## 6 Epuka Vikwazo

Wakati wa mazungumzo, mwanamke huyo alileta tofauti za kijamii vyombo vya kuchotea maji, mababu zake, na tofauti katika ibada. Lakini Yesu aliendelea kurudi kwa hitaji la mwanamke huyo - kumjua Yeye.

Baada ya kuanza kumjadili Yesu, usikengeushwe na mambo mengine. Endelea kuyarudisha mazungumzo ili kuzungumza juu yake Yesu.

Andika mawazo kadhaa ya kurudisha mazungumzo Kristo ikiwa itatoka nje.

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

## 7 Usikunjane chini ya Shinikizo

Yesu kakuacha mazungumzo yalipopata mvutano kidogo, hata hivyo Yeye kamwe hakumlazimisha mwanamke kumsikiliza dhidi ya mapenzi yake. Katika kuzungumza na marafiki zako, chukua mazungumzo kadri uwezavyo kuelekea katika kumuongoza mtu mwingine kwa Kristo, lakini kamwe usifikiekiwango cha ufidhuli au kutokuwa na hisia. Hata hivyo, kwamba mtu mwingine anahisi wasiwasi kidogo haimaanishi kuwa ni wakati wa kuacha mazungumzo. Endelea kuwasiliana.

Ukibaki kuwa makini kwa Roho Mtakatifu, utajua umbali wa kuyapeleka mazungumzo.

Kwa ubunifu fikiria juu ya vidokezo ambavyo vitakusaidia kujua kama kuacha au kuendeleza mjadala kumhusu Yesu.

## 8 Zungumza kwa Ubunifu

Tunapojua majibu, tutakuwa na ujasiri zaidi katika imani yetu, na kwa hiyo, mashahidi wajasiri. Pia, tutakuwa na vifaa bora zaidi vya kusaidia wasio Wakristo wamwelewe Yesu na athari Anazoweza kuwa nazo katika maisha yao.

**Soma Matendo 17:1-4**. jinsi gani Paulo aliwashawishi watu kwa ukweli wa Yesu Kristo? Ni masomo gani unaweza kujifunza kutoka uzoefu wake?

| Alichokifanya Paulo | Ninachoweza kujifunza |
| --- | --- |
| ____________________ | ______________________ |
| ____________________ | ______________________ |
| ____________________ | ______________________ |
| ____________________ | ______________________ |
| ____________________ | ______________________ |

Baadaye Paulo alisafiri hadi Athene na kukutana na watu wa asili aina mbalimbali

**Soma Matendo 17:16-21** na ueleze kilichotokea.

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Waepukurea walikuwa kikundi cha watu waliotafuta raha

katika kila kitu walichokifanya. Lengo lao kuu na kipaumbele chao kikuu kilikuwa raha. Wastoa waliamini kwamba watu wanapaswa kuepuka kuonyesha hisia zozote, ikiwemo  mwitikio wowote wa furaha au dhiki.

Baadhi ya falsafa za maisha ambazo marafiki zako wanazo tofauti na yako ni zipi?

**Soma Matendo 17:22-31**. Paulo aliwafikiaje wasikilizaji wake waliositasita?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

Tunaweza kujifunza nini kutoka kwa Paulo kitakachotusaidia kuitikia kwa watu wanaofikiri tofauti na sisi?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

**Soma Matendo 17:32-34**. Baada ya Paulo kusema, watu walijibuje? Unadhani watu watakujibu vipi?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

## JINSI YA KUJIBU

Wakati watu wanauliza maswali magumu, wakati mwingine hatujui jinsi ya kuwajibu. Chaguo mojawapo ni kubishana nao au kutetea majibu yetu kwa kumpiga mtu mwingine juu ya kichwa na Biblia ya King James yenye uzito wa pauni hamsini.
Chaguo lingine ni kutambaa kwenye shimo. Lakini hebu tuangalie baadhi ya majibu bora zaidi.

- *Kuwa mwaminifu*. Kumjua Yesu Kristo haimaanishi kuwa utajua jibu la kila swali lililoulizwa kumhusu. Kama huna jibu mara moja, ahidi kuliangalia na kumrudia huyo muulizaji. Wakati mwingine mtu mwingine akiuliza swali

sawa na hilo, utajua jibu.

- *Usibishane kamwe*. Unajaribu kumwongoza mtu kwa Kristo, si kushinda mjadala. Yesu alisemezana na watu kuhusu mambo waliyoyaamini. Hakubishana nao kamwe.

- Sikiliza kwa makini. Lazima ujifunze kusikiliza kwa makini ili kugundua hali ya kiroho ya mtu mwingine. Angalia zaidi ya maswali yake na upate mahitaji yake halisi.
- Endelea kufuatilia. Mara nyingi watu hukatiza unachosema kwa maswali ambayo hayapo kwenye mada. Hili likitokea, ahidi kujadili maswali yao mara tu unapomaliza kushiriki maswali yako juu ya Yesu Kristo.

Shughulikia maswali ya dhati ili kufafanua kuchanganyikiwa ambako mtu mwingine anaweza kuwa nako, lakini ahirisha maswali ya "kielimu" ambayo hutumiwa kama kizuizi ili kukwepa suala halisi la Yesu Kristo.

## UJIBU NINI

Maswali yafuatayo ni yale yanayoulizwa zaidi na wanafunzi kumhusu Yesu. Ikiwa unajua majibu ya maswali haya, wewe utaweza kukabiliana na karibu pingamizi yoyote ambayo mtu yeyote atainua unaposhiriki imani yako. Baada ya kila swali, wewe utapata majibu yaliyopendekezwa ili kuchangamsha mawazo yako.

### 1 Je, Mungu yupo?

Hoja za uwepo wa Mungu ni pamoja na:

- *Imani ya uwepo wa Mungu ulimwenguni*. Sosholojia na akiolojia zinaonyesha ushahidi mwingi wa imani katika Mungu mmoja mkuu. Watu wengi wa asili mbalimbali na hata wasio na elimu wanamwabudu Mungu kwa njia fulani. Watu wengi katika historia wameamini katika Mungu au aina fulani ya mungu au miungu.
- *Sheria ya athari na sababu zake*. Hii sheria ya kisayansi inasema kwamba hapana athari inayotolewa bila sababu. Binadamu na ulimwengu wenyewe ni athari zinazoelekeza kwenye sababu. Chanzo cha hizi "athari" ni Mungu Mwenyewe, Ndiye "Sababu" kuu.

- *Utaratibu na muundo wa ulimwengu*. Ushahidi wa ubunifu u kila mahali. Haiwezekani kwamba ulimwengu uliumbwa kwa kwa bahati mbaya ya "mlipuko mkuu" Ni kama ilivyo vigumu tumbili anayecheza kwenye kompyuta kukusudia kuandika anwani ya mtu. (Soma Zaburi 19:1-4; Warumi 1:19-20.)
- *Umwilisho*. Mungu asiyeonekana "huko nje juu" alichagua kuwasiliana na watu "chini hapa." Alifanya hivi kwa kumtuma Yesu Kristo katika umbo la mwanadamu kuishi nasi. Tuseme kama wewe unaendesha gari na unakaribia nyumbani na kwenye barabara yako, unaona kichuguu, lakini hutaki kuwaumiza mchwa. Utafanya nini ili wakuitike na watoke barabarani? Unaweza piga kelele, uwaandikie barua, au hata uwapeperushie bendera, lakini huwezi kuwasiliana nao isipokuwa ufanyike chungu. Wakati Yesu alikuja duniani kama Mwanadamu, aliweza kutufunulia upendo wa Mungu.
(Soma Yohana 1:18 na Waebrania 1:1-2.)

- *Maisha yaliyibadilishwa*. jinsi gani tunaweza kueleza mabadiliko makubwa na ya kudumu katika maisha ya wafuasi wa Yesu kama si Yesu Kristo? Maisha yaliyobadilishwa, yakiwa ni pamoja na yako, yanaweza kuwa ya kibinafsi zaidi na kielelezo chenye nguvu kwa mtu mwingine, cha ukweli kwamba Mungu yupo.

## JIBU LANGU

Sasa tuseme rafiki anakuuliza, "Unajuaje Mungu yupo?" ungemjibuje?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

**2 Je, Ikiwa Siamini Biblia?**
Ikiwa mtu atauliza swali hili, mwambie afafanue kwa kumuuliza maswali mawili yako mwenyewe:
"Je, huamini kwamba Biblia ni Neno la Mungu?"

"Je, unaweza kunionyesha makosa yoyote katika Biblia?"

Chukua hatua ya kwanza na uonyeshe kwamba Biblia ni hati ya kihistoria inayotegemeka na ambayo inaweza kuaminiwa. Hapa kuna ukweli wa kuunga mkono jibu lako:

- **Biblia inadai kuwa Neno la Mungu**. Mara tena na tena, waandishi wa Biblia wanatumia msemo "Bwana asema…" ili kuonyesha kwamba Mungu ndiye mwenye mamlaka ya uandishi huo.

- **Biblia imeongozwa na roho wa Mungu** (2 Timotheo 3:16-17). Neno, kuongozwa na roho maana yake ni "kupuliziwa na Mungu," kwa hiyo kila neno lake limekuja kutoka kwa Mungu.

- **Waandishi wa Biblia walikuwa mashahidi waliojionea kwa macho** (2 Petro 1:16). Waliandika kile ambacho walijua kabisa kuwa ni kweli na walikishuhudia.

- **Biblia hupita majaribio yote ya usahihi** wa kihistoria.

Je, hati inaweza kuamuliwaje kuwa sahihi kihistoria? Katika kitabu cha *Ushahidi Ziada Unaodai Uamuzi* (Here's Life), Josh McDowell anavinukuu vipimo vinne kulingana na C. Sander:

1. *Jaribio la wasifu* Je, miswada inategemeka kwa kiasi gani? Ni muda kiasi gani umepita kati ya hati ya asili na ya zamani zaidi ambayo inapatikana?

Hakuna anayehoji kutegemeka kwa hati za Kaisari zinazorekodi Vita vya Gaelic vya mwaka wa 58 kabla ya Kristo. au maandishi ya mwanahistoria Mroma Tacitus. Hata hivyo hati za mapema zaidi kuwapo zimeandikwa kuanzia miaka 600 hadi 1,000 baada ya hati za awali kuandikwa. Kwa maneno mengine, hati asilia ilinakiliwa, kisha nakala hiyo ikanakiliwa, na kuendelea na kuendelea na kuendelea kwa mamia ya miaka. Sasa ziliopo ni hati chache tu ambazo zimenakiliwa tena na kupitishwa kwa karne nyingi. Hata hivyo, wanahistoria wanaamini kwamba hati hizo ni zenye kutegemeka.

Wanahistoria hawajapata maandishi machache tu ya kuunga mkono Agano Jipya, - wamepata maelfu ya maandishi. Mifano miwili bora kutoka kwa karne ya nne ina Agano Jipya lote, na zingine zina sehemu za Agano Jipya ambazo ziliandikwa kuanzia A.D. 200-300. Kipande kimoja cha kitabu cha Yohana kiliandikwa mapema kama A.D. 130. Wakati inakuja kwa usahihi wa kihistoria, hakuna mtu anayeweza kuhoji uhalali wa Agano Jipya.

2. *Uchunguzi wa ushahidi wa ndani*. Mtihani huu unahusiana na muandishi na mtindo ili kuamua uegemeaji. Je, ushuhuda wa hao waandishi unaweza kutegemewa?

Mamlaka ya waandishi wa Agano Jipya yanathibitishwa na ukweli kwamba kwa hakika walimjua Yesu au walikuwa mashahidi waliojionea kazi Zake. Kwa sababu wanafunzi waliishi na kuandika wakati ambapo wakosoaji wao walikuwa kila mahali, wakosoaji hao wangefurahia kuwafichua kuwa wadanganyifu - hasa juu ya somo la ufufuo. Ikiwa mitume walisema uwongo kama walivyoandika Biblia, maelfu ya mashahidi waliokuwa hai wangefichua kama ulaghai, na Ukristo ungeisha papo hapo hata kabla haujaanza. Agano Jipya linategemeka kwa sababu waandishi waliweza kuunga mkono ushuhuda wao kama mashahidi waliojionea kwa macho. (Tazama Luka I: I-3; Matendo 2:22; na I Yohana 1:3.)

3. *Uchunguzi wa ushahidi wa nje* Ushahidi wa nje unatoa msaada kutoka vyanzo vingine isipokuwa waandishi wa Agano Jipya ili kuthibitisha kutegemewa kwa Agano Jipya. Chanzo kimoja kama hicho ni maandishi ya mapema ya akinababa wa kanisa. Kuna idadi kubwa ya nyenzo zinazojitegemea ambazo zinanukuu kutoka kwa Agano Jipya. Baadhi ya akinababa waandishi hao ni pamoja na Clement (A.D. 95), Ignatius (A.D. 70-110), Polycarp (A.D. 70-156), na Irenaeus (A.D. 180).

Ushahidi mwingine wenye nguvu wa nje ni akiolojia. Hii sayansi ya kuchimbua masalio ya kale haijakosa kamwe kuthibitisha Biblia. Kulingana na Nelson Glueck, mwanaakiolojia mashuhuri wa Kiyahudi, " Hapana ugunduzi wowote wa kiakiolojia umewahi kupinga marejeleo ya kibiblia."

4. *Mtihani wa unabii uliotimia*. Kiwango cha kibiblia kwa

nabii wa kweli kilikuwa usahihi wa asilimia 100 ( Kumbukumbu la Torati 18:21-22 ). Wengi wa Manabii wa Agano la Kale walinena juu ya Masihi ajaye. Zaidi ya 300 kati ya hizo nabii zilitimia kupitia kwa Yesu. Kulingana na Peter Stoner (*Sayansi Inanena*, Moody Press), "Uwezekano kwamba mtu ye yote angeishi wakati wa sasa na atimize unabii nane ni takribani 1 kwa 100,000,000,000,000,000). Stoner anaendelea kufafanua hilo.

Dola za sarufi 10 zinaweza kupangwa kwa kina cha futi mbili katika jimbo zima la Texas. Tuseme umeweka alama juu ya moja tu kati ya hizo dola za sarufi, ukaificha na kumfumba macho mtu wa kujitolea. Mtu huyo angekuwa na nafasi kama hiyo kuichagua dola hiyo sahihi kwa chaguo moja. Hata hivyo, Yesu alitimiza si unabii 8, bali zaidi ya 300!

## JIBU LANGU

Sasa, bila kuangalia nyuma, eleza kwa ufupi jinsi ungemjibu rafiki anayetilia shaka mamlaka ya Biblia.

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

## 3 Je, Yesu ndiye njia ya pekee kumuelekea kwa Mungu?

Baadhi ya watu wanatilia shaka madai ya ukristo kuwa ndiyo njia pekee ya kumfikia Mungu. Wanabainisha kuwa Waislamu na Wayahudi ni waaminifu katika imani yao. Wakristo wanashutumiwa kuwa na mawazo finyu juu ya jambo hili, bado sisi, kama waumini, inabidi tuiache Biblia ijisemee na kujitetea yenyewe.

- Yesu alisema, “Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi” (Yohana 14:6).
- Petro (na mitume wengine) walifundisha kwamba, “Wokovu haupatikani ndani ya mtu

mwingine [isipokuwa Yesu Kristo], kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo”

- ( Matendo 4:12 ).
- Yesu anatufunulia Mungu (Yohana 1:18).
- Yesu anawezesha kuwa na uhusiano wa kibinafsi na Baba (1 Petro 3:18).

- Hakuna kiongozi mwingine wa kidini aliyewahi kufufuka kutoka kwa wafu. Makaburi ya Muhammad, Buddha, Confucius, na wengine wengi ambao walianza harakati za kidini zote zina maiti. Yesu Kristo pekee ndiye alishinda kifo, na kupitia Yeye tu, uzima wa milele unawezekana.

## JIBU LANGU

Sasa fanya muhtasari wa jinsi unavyoweza kumweleza mtu kwamba Yesu Kristo ni njia ya pekee ya kwenda kwa Mungu.

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

## 4 Je, Yesu Aliweza Vipi Kufufuliwa kutoka kwa Wafu?

Ushahidi wa kufufuka kwa Yesu ni mwingi. Fikiria uthibitisho ufuatao:

1. *Ushahidi wa wasomi*. Uwasilishaji rahisi wa ukweli wa kifo cha Yesu na ufufuo umewasadikisha watu wengi wenye hekima zaidi duniani kwamba hakika Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.
Mfano mmoja ni Bwana Lindhurst, mmoja wa wanasheria mwenye mamlaka makubwa katika historia ya Uingereza. Lindhurst anaandika, "Ninajua vizuri ushahidi ni nini; na Ninakuambia ushahidi kama huo wa Ufufuo haujawahi kuvunjwa” (*Kwa hiyo Simama*: Christian Apologetics, Wilbur M. Smith, iliyotajwa na Josh McDowell katika *Ushahidi Unaopasa Uamuzi*, Campus Crusade for

Christ).

Mfano mwingine ni profesa wa sheria wa zamani wa chuo kikuu cha Harvard, Simon Greenleaf. Akipigwa changamoto na wanafunzi wawili kuhusu kama Ufufuo ungesimama kwenye mahakama ya sheria, Greenleaf alijibu ndiyo. Baada ya utafiti wa kina, Greenleaf alihitimisha, "Ufufuo wa Yesu Kristo ndio ukweli mkuu Zaidi uliowahi kuthibitishwa na historia" (Ushuhuda wa Mwinjilisti, Baker).

2. *Nguo za kaburi ambazo hazikuwa na usumbufu* (Yohana 20:1-8). Petro na Yohana walipoyaona mavazi ya kuzikiwa Yesu, waliona vitambaa vya kitani lakini hapakuwa na mwili. kitambaa cha kichwa kilikuwa pale na "kilijikunja chenyewe." Wakiwa na ushahidi huu mbele yao, "waliona na kuamini."

*3 Kaburi tupu*. Wenye mamlaka walichukua tahadhari kubwa kuzuia kutoweka kwa mwili wa Yesu.

- Yesu aliwekwa katika kaburi jipya lililochongwa kutoka kwenye mwamba imara ( Mathayo 27:60 ). Mwili wa Yesu ulikuwa umefungwa kwa vitambaa vya kitani na manukato kilo karibu 75 hivi ya kuzikia (Yohana 19:39-40).

- Kaburi la Yesu lilifungwa kwa jiwe kubwa lenye uzito wa tani mbili ( Mathayo 27:60 ).

- Viongozi wa Kiyahudi walifanya kaburi hilo kuwa chini ya ulinzi kwa kulitia muhuri wa Pilato kwenye jiwe (Mathayo 27:60). Nembo rasmi ya mfalme kwenye kaburi hilo ilimaanisha kifo kwa yeyote aliyelivunja.

- Warumi waliweka walinzi kulizunguka kaburi (Mathayo 27:65). Hawa walinzi walikuwa ni askari 16 waliopata mafunzo bora Zaidi duniani.

Ingawa ufufuo wa Yesu ulihitaji kulishinda kaburi, sanda, manukato, muhuri, viongozi wa Wayahudi na walinzi wa Kirumi; hakuna kinachomshinda Mungu. Kwa kweli, maelezo pekee ya busara wakati Mwili wa Yesu ulikosekana ni kwamba Yesu Kristo alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Hakuna maelezo mengine

yanayolingana na ukweli wote.

4. *Mionekano kumi*. Yesu alionekana angalau mara 10 tofauti katika siku 40 baada ya kufufuka kwake na kuonekana na watu kama 500. Yeye alikula samaki. Aliongea. Baadhi ya wanafunzi wakamgusa. Mistari ifuatayo ina marejeleo ya kuonekana kwa Yesu baada ya kufufuka: Mathayo 28:9-10, 16-20; Marko 1:14; Luka 24:13-32, 34,36-43; Yohana 20:14,26-29; 21:1-23; 1 Wakorintho 15:6-7.

5. *Maisha ya wanafunzi yaliyobadilika*. Yesu alipokuwa hai, familia yake na marafiki zake hawakuelewa kwa hakika kile alichokuwa anajaribu kuwafundisha kuhusu kifo na ufufuo wake. Wakati fulani, wanafamilia Yake hata walifikiri kuwa alikuwa “amerukwa na akili” ( Marko 3:20-21 ). Lakini baada ya kufufuka, wafuasi wa Yesu walianza kuelewa kilichotokea. Wanafunzi wake walianza kunena kwa ujasiri na nguvu, na ndugu yake mwenyewe, Yakobo, alianzisha waraka wake kwa maneno haya, “Yakobo, mtumishi wa Mungu na wa Bwana Yesu Kristo” (Yakobo 1:1).

*6 Maisha ya watu yaliyobadilika kwa karne nyingi*. Mamilioni ya watu wamebadilishwa na Yesu Kristo katika takriban miaka 2,000 baada ya ufufuo Wake. Na wengi wasioamini, ambao wana mwelekeo wa kupuuza ushahidi wa historia, wamemjua Yesu Kristo kwa sababu mtu fulani waliyemjua aliiga mtindo wa kweli wa maisha ya Kikristo.

**Uwepo wa Yesu Kristo katika maisha yako inaweza kuwa ndio ushahidi borazaidi wa ufufuo ambao unaweza kumpa rafiki yako.**

## JIBU LANGU

Sasa, eleza kwa ufupi kutoka kwa kumbukumbu kile ungemwambia mtu ambaye anataka kujua jinsi gani unaweza kuamini kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.

## 5 Je, Mungu Mwema Awezaje Kuwapeleka Watu Kuzimu?

Ikiwa hakimu anawapeleka watu wenye hatia jela, hakuna anayemshtaki kuwa hakimu mbaya. Anafanya tu yaliyo haki. Hata hivyo baadhi ya watu wanafikiri Mungu ni mbaya au si wa haki kwa sababu Anasema kwamba watu wenye hatia watahukumiwa. Wakati unawashughulikia watu wanaoshikilia haya maoni, wasaidie kuelewa ukweli:

- Mungu ni mwenye haki (Ayubu 34:12). Haiwezekani Yeye kudhulumu.

- Mungu hutoa ushahidi wa kutosha juu yake mwenyewe kupitia kwenye mazingira ili watu wamwitikie (Warumi 1:19-20)

- Mungu hawawajibikishi watu kwa yale wasiyoyajua. Ikiwa una Biblia na una uwezo wa kusoma, unawajibika kutii amri za Mungu zilizoandikwa katika Maandiko. Lakini kwa wale walio mbali katika maeneo ya ulimwengu ambapo Biblia (na kusoma) haijulikani, Mungu hawahukumu watu kwa jinsi wanavyoishi vizuri kwa kushika vizuri Amri Kumi. Badala yake, Anajitambulisha kupitia dhamiri zao (Warumi 2:12-16).

- Watu wote wamepokea kiasi Fulani cha nuru, unaweza kuona kidogo kwa mwanga wa nyota. Unaweza kuona vizuri Zaidi kama mwezi kamili umetoka. Lakini mwanga bora ya yote ni jua. Watu hupokea kiasi tofauti cha "nuru" ya Mungu, na wanatarajiwa kujibu kwa kiasi cha mwanga ambacho wamepokea. Wakati wao wanachagua kukataa nuru hiyo, wanatembea katika giza na hukumu ( Yohana 3:19-21 ).

- Hakuna awezaye kuokolewa isipokuwa kwa Yesu Kristo (Yohana 14:6; Matendo 4:12). Yesu

ndiye njia pekee ya kwenda kwa Mungu.

- Mungu hataki kumpeleka mtu kuzimu (2 Petro 3:9). Kuzimu iliumbwa kwa ajili ya shetani na malaika wake (Mathayo 25:41). Mungu anataka watu wote watubu na kuishi naye milele.

### JIBU LANGU

Tuseme rafiki akuulize jinsi Mungu mwema anavyoweza kuwapeleka watu motoni.

Andika jibu lako hapa chini kutoka kwa kumbukumbu.

____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

**6 Je, Mimi sitakwenda Mbinguni Nikiwa Mwema?** Mungu hapendi viwango! Wokovu wa mtu ni ndio au la.

Mtu anapomwamini na kumpokea Yesu Kristo kama mwokozi wake binafsi, "anapita - ndio" na amehakikishiwa mbingu. Kama hafanyi uamuzi huo, kamwe haiwezekani kwake kuwa "mzuri wa kutosha" kuingia mbinguni. Yeye "anashindwa - la." Fikiria hoja ifuatayo:

— Inawezekana kuwa mtu mzuri bila kuwa Mkristo. Nikodemo alikuwa Myahudi mwenye elimu ya juu, tajiri na kiongozi mwenye maadili, lakini Yesu alimwambia, “Lazima uzaliwe mara ya pili” (Yohana 3:1-7).

— Maisha mazuri ya kiadili hayawezi kumuokoa mtu yeyote. Kiwango cha Mungu ni utakatifu kamili. Ikiwa tuna hatia ya dhambi hata moja, hatuwezi kuingia katika uwepo wa Mungu kwa msingi wa “wema” wetu (Yakobo 2:10).

— Yesu alikuja duniani kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Kama tungekuwa nao uwezo wa kuwa mzuri vya kutosha ili kufika mbinguni (na kwa Mungu) kwa nguvu zetu wenyewe, basi Mungu

asingemtoa Mwanawe Yesu kuwa dhabihu kwenye msalaba. Hilo lisingalikuwa jambo la lazima ( Waefeso 2:8-9; Tito 3:5).

Mtu yeyote anayefikiri kuwa ana wema wakutosha ili kufika mbinguni pengine ana tatizo la kiburi. Kuona tu kutoka kwa mtazamo wa Mungu kutabadilisha akili ya mtu kama huyo (Zaburi 10:4).

## JIBU LANGU

Ungemwambia nini mtu anayeuliza, "Je, siendi mbinguni ikiwa mimi ni mtu mzuri?"

## 7 Kwanini Mungu Anaruhusu Uovu na Mateso?

Hili ni swali gumu kujibu. Hata hivyo ikiwa kuwepo kwa uovu hutufanya tufikiri kwamba hakuna Mungu, tuna tatizo kubwa zaidi.
Dostoevski, mwandishi wa riwaya wa Kirusi, alisema, "Ikiwa hakuna Mungu, basi chochote kinaruhusiwa. Basi ”kwa kudhania kwamba Mungu yupo, kwa nini Yeye anaruhusu uovu?

— Ulimwengu ambao Mungu aliumba ulikuwa mkamilifu, lakini wanadamu walipewa uhuru wa kutomtii Mungu. Uovu ulikuwa ni matokeo ya mwanadamu kutotii (Mwanzo 3:22).

— Uovu ni wa muda. Yesu Kristo alikufa msalabani ili kutatua tatizo la uovu (Isaya 53:4-6). Uovu utakuwa tatizo la muda tu wakati tuko katika ulimwengu huu (Ufunuo 21:4).

—Wema wa Mungu ni mkuu kuliko uovu tunaokabiliana nao. Mungu anahusika katika mateso na uchungu wetu. Anatujali (2 Wakorintho 1:3-5; 1 Petro 5:7).

—Uovu hutufanya tuone kutokuwa na tumaini kwetu na kumgeukia Mungu.

**JIBU LANGU**

Sasa, kutoka kwa kumbukumbu, andika jinsi unavyoweza kuelezea uwepo wa uovu kwa rafiki anayekuuliza.

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

**Baada** ya marafiki kuuliza maswali yao, nawe wape maswali manne ya kufikiria.




**Maswali 4**

**1. Yesu Kristo ni nani? Kulingana na madai ambayo alitoa, kuna chaguzi nne tu: Alikuwa mwongo, kichaa, hodari, au Bwana.**

**2. Je, unaelezaje Yesu kufufuka kutoka kwa wafu? Ushahidi wa ufufuo ni mwingi sana. Mzigo wa ushahidi u juu ya asiyeamini athibitishe kinyume cha ukweli huu!**

**3. Je, na iwapo umekosea? Kafiri atapoteza kila kitu kwa kukosa kuyatoa maisha yake kwa Yesu Kristo.**

**4. Ikiwa ungesadikishwa kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, je! ungeyatoa maisha yako kwake? Watu wengine hutumia maswali kuficha hofu zao kuhusu kukabiliana na Kristo kibinafsi. Swali hili hulenga hapo na kupata mahitaji yao halisi.**

**Hoja za kiakili haziwavui watu, inagharimu upendo wa Yesu Kristo ukitiririka kupitia kwako!**

Rudia maswali katika somo hili la Biblia mara kadhaa. Kariri majibu kwa kila swali. Ongeza vidokezo vyako mwenyewe, vielelezo, na Maandiko. Kutana na rafiki Mkristo na pitia kila swali mpaka kila muhtasari uwe wazi akilini mwako. Kisha weka muda wiki hii kuzungumza na rafiki ambaye anatatizika na mojawapo ya maswali haya. Kabiliana na swali moja kwa moja. Rekodi matokeo ya mkutano wako hapa chini.

**Kamilisha sehemu hii kwa kukariri Ufunuo 3:20.**

## KAZI

1. Endelea na nyakati zako za kila siku peke yako na Mungu, ukitumia masomo yafuatayo:

    Siku ya 1: Matendo 23:12-35

    Siku ya 2: Matendo 24:1-9

    Siku ya 3: Matendo 24:10-27

    Siku ya 4: Matendo 25:1-12

    Siku ya 5: Matendo 25:13-27

    Siku ya 6: Matendo 26:1-11

    Siku ya 7: Matendo 26:12-32

**2. Kamilisha Sehemu ya 10.**

3. Shiriki ushuhuda wako na umuwasilishie Injili rafiki

asiyeamini wiki hii.

4. Endelea kupitia maswali na majibu kutoka katika somo hili la Biblia. Kutana na mtu mmoja ambaye anapambana na mojawapo ya maswali haya na muyazungumzie.

## SEHEMU YA 10




## Kumsaidia Mkristo Mchanga Kukua

Baada ya mazungumzo mengi na Andy, Yohana amempokea Kristo na ana hamu kubwa ya kukua katika uhusiano wake na Yesu. Andy amesisimka. Anataka kumshuhudia kila mtu! Kwa hivyo anaanza kutumia wakati na mtu mwingine ambaye ni rafiki asiye mkristo huku akimuacha Yohana peke yake. Hamuoni Yohana sana isipokuwa mara kwa mara shuleni. Wakati Andy na Yohana hatimaye wanaketi chini na kuzungumza tena, Andy anagundua kwamba Yohana amepoteza msisimko wake kwa ajili ya Kristo.

Je, Andy angefanya nini ili kumsaidia Yohana kukua kama muumini mpya na kubaki na shauku ya kumfuata Yesu?

**WANAKUAJE?**

Unapomwongoza rafiki kwa Kristo, unapata fursa na wajibu wa kuona kwamba rafiki yako anakua. Kama "mzazi wa kiroho," wewe usije kudhani kwamba anaweza kujilisha na kujijali mwenyewe. Ni nini kinachohitajika na watoto wachanga na waumini wapya? Kwa nini? ( 1 Petro 2:2 )

Mahitaji ya Wakristo wapya ni sawa na yale ya watoto wachanga. Wote wanahitaji mtu wa kuwalisha na kuwatunza. Hebu tuangalie baadhi ya mahitaji hayo.

**1 Upendo**

Mkristo mpya anahitaji kupata uzoefu wa usalama na kukubalika. Hiyo inatokana na kupendwa. Upendo wa kweli unazidi kuzungumza tu; inajumuisha matendo pia. **Soma 1 Yohana 3:16-18.** Ni kwa njia gani tunaweza kuweka upendo wetu katika matendo na mwamini mpya?

**2 Chakula**

Waumini wapya hutegemea kabisa mtu mwingine kuwalisha. Hapana mtu anatarajia mtoto mchanga kwenda jikoni na kupika mayai kwa kifungua kinywa. Lakini wakati mwingine tunafikiri Mkristo mpya anajua jinsi ya kula chakula cha kiroho.

**Soma 1 Timotheo 4:6**. Nini baadhi ya njia ambapo unaweza kusaidia kumlisha na kumkuza mwamini mpya?

**3 Kuitika**
Wakristo wachanga na watoto wadogo ni kama kondoo. Linapokuja swala la kujilinda, wako hoi.

**Soma 1 Petro 5:8 na Waefeso 6:10–17**.
Waumini wapya wanahitaji kulindwa kutoka kwa nini? Wanawezaje kujifunza kujilinda wenyewe?

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

**4 Mafunzo**
Haitoshi kwa mzazi kumpenda, kulisha na kumlinda mtoto. Mtoto lazima afunzwe.

**Kulingana na Wakolosai 2:7**, ni aina gani ya mafunzo waumini wapya wanahitaji?

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

Wakristo wachanga wanahitaji kuzoezwa katika mambo mengi kama kumjua Yesu Kristo, maombi, kujifunza Biblia, ushirika, kushuhudia, na utii kwa Mungu. Wakipata mafunzo katika maeneo haya ya msingi, wanaweza kuwa imara katika imani yao.

## KWANINI MIMI?

Kuyakidhi mahitaji ya waumini wapya ili kuwasaidia kuishi kwa ajili ya Kristo, inadai kujitolea kwa upande wetu. Fikiria baadhi ya sababu nzuri ili tujikabidhi kwa jukumu kubwa kama hili:

*Ikiwa tunashiriki katika kuzaliwa kiroho basi tunawajibika ukuaji wa kiroho*. Mtume Paulo alichukua safari za umishonari kwenda kuhubiri na kuyaanzisha makanisa mapya. Lakini hakuishia hapo. Angeweza kurudi nyuma mara mbili baadaye na kuangalia juu ya ukuaji wa makanisa mapya (Matendo 14:21-28). Wakati mwingine hakuweza kumtembelea mtu, hivyo aliandika barua (1

Wakorintho 16:21; Wagalatia 6:11). Na Paulo kila mara aliwasaidia ndugu na dada zake wapya katika Kristo kwa kusali kwa ajili yao (Wakolosai 1:3-4,9-12). Kutokana na aya hizi, ni mambo gani maalum unaweza kufanya ili kumfuata mwamini mpya?

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

*Kama viungo vya mwili wa Kristo sisi sote tunayo nafasi ya kuwasaidia waumini wachanga kukua*. Mtume Paulo alielezaje jukumu hili? ( Waefeso 4:11-16 )

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

*Ikiwa tunampenda Yesu, tutawatunza walio wake*. Kuwapenda wakristo wachanga huthibitisha kwamba tunampenda Yesu.
Yesu alimwambiaje Petro jambo hilo?
( Yohana 21:15-17 )

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

*Yesu alituamuru kufanya wanafunzi kutoka kwa mataifa yote* (Mathayo 28:18-20). Kuwafanya wanafunzi si sawa na kuwafanya waongofu. Kuafanya wanafunzi kunahusisha “kuwafundisha kutii kila kitu” ambacho Yesu alifundisha. Tunaweza kufanya nini ili kuwasaidia watu kuwa wafuasi thabiti wa Kristo kulingana na Mathayo 28:18-20?

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

Changamoto yetu ya "kumleta kila mtu mkamilifu katika Kristo" (Wakolosai 1:28) ni jukumu kubwa, lakini pia ni

fursa kubwa. Inasisimua kutafakari jinsi Mungu anavyotaka kututumia kuwajenga ndugu na dada zetu wadogo katika Kristo.

**TUNAANZAJE?**

Kwa muda wa masaa yasiozidi 48 baada ya rafiki yako kumpokea Kristo, fuata hatua hizi kwa usahihi kumtoa rafiki yako "nje ya vizuizi" hadi kwenye barabara ya kwenda katika uhusiano wa kusisimua, unaokua kwa Yesu.

1. *Rudia Uamuzi*. Pitia uwasilishaji wa Injili tena. Soma maombi tena. Thibitisha kwamba rafiki yako amempokea Yesu Kristo. Omba na kumshukuru Mungu tena kwa yale ambayo Yesu amefanya.

*2.Toa Changamoto*. Mwambie kwamba unataka kumsaidia kukua katika upya wake wa uhusiano na Yesu. Soma pamoja Wakolosai 2:6-7. Zungumza kuhusu kukuza bustani. "Tuseme umepanda tu mbegu kwenye bustani, nini itatokea ikiwa hautawahi kumwagilia maji, kupalilia, au kutia mbolea?
Lakini kwa kumwagilia, palilia, na kutia mbolea itakua. Ndivyo ilivyo katika uhusiano wako pamoja na Kristo". Muulize kama atakutana nawe mara moja au mbili kila wiki kwa majuma sita yajayo ili kuzingatia ukuaji wake katika Kristo. Mwambie kuwa mtafanya kazi pamoja, lakini itagharimu kazi fulani kwa upande wake.

*3. Kuwa mkweli* Eleza kwamba wewe si mkamilifu na hujui majibu yote. Tafuta majibu katika Biblia. Weka wazi kwamba unaweza kutomridhisha na hata kumvunja moyo. Mtakumbana na vikwazo, lakini hamuwezi kuacha kumpenda Yesu au nyinyi kwa nyinyi.

5. Tumia kitabu cha *'Kuanza'*. Agiza nakala ya *Kuanza* kwa ajili yenu nyote.

   Mwambie kwamba hivi ndivyo mtakavyojadili.

Tenga wakati na mahali pa kukutania. Kumbuka kumpigia simu umkumbushe kabila ya wakati.

***Kuanza*** ni kitabu kinachopatikana kutoka
Reach Out Youth Solutions
www.reach-out.org au I -800-473-9456

**TUFANYE NINI?**
Mkristo mpya anahitaji kuungwa mkono, kutiwa moyo, sala, na nafasi ya kuzungumzia imani yake na Mkristo mwingine. Akizungumza kuhusu Biblia na kujibu maswali katika kitabu *Anza* kutamsaidia rafiki yako kukua kiroho. Weka mawazo haya akilini unapokutana:

- *Mwambie nini*? Mwambie lengo la kikao na ni nini yeye anapaswa kujua unapomaliza.
- *Mwambie kwanini*? Mpe majibu kutoka kwa Maandiko na kutoka uzoefu wako na Kristo.
- *Mwonyeshe jinsi gani*. Mwonyeshe kwa vitendo jinsi unavyotumia mawazo katika kitabu cha *Kuanza*. Kwa mfano, mwonyeshe unachofanya unaposoma Biblia na kuomba.
- *Msababishe kupiga hatua*. Kutana naye ili kufanyia kazi somo pamoja. Hakikisha nyote wawili mnaifanya tofauti, kisha mjadili pamoja.
- *Ipitishe*. Msaidie kuwaelezea wengine yale anayojifunza kumhusu Yesu Kristo. Nenda naye kufanya hivyo. Muda si mrefu ataanza kuwaongoza watu wengine kwa Kristo. Hii ni aina ya uzazi wa kiroho ambao Yesu alikuwa nao akilini mwake alipotupa Agizo Kuu ( Mathayo 28:18-20 )

Fuata muundo huu ili kufaidika Zaidi kutokana na majadiliano.




1. Tumia dakika chache kupata kujuliana hali ya maisha ya kila mmoja.

2. Nenda kupitia kila sehemu na ujibu kila swali. Angalia kila mstari wa Biblia na kuuzungumzia. Hakikisha unafanya kila sehemu mwenyewe.

3. Mwambie afanye muhtasari wa kila jambo katika kipindi.

4.Jadili jinsi kipindi kinavyotumika katika maisha yako ya kila siku. Msaidie kuwa mahususi katika maombi yake.

6. Pitia mstari wa kumbukumbu pamoja. Tumia miongozo hii kumsaidia ajifunze:

- nukuu mada na marejeleo mwanzoni na mwisho wa mada
- Jifunze kishazi kimoja kwa wakati mmoja na urudie hadi utakapokijua, ndipo ukiendee kifungu kifuatacho.
- rudia mstari kila siku juma hilo.

6. Ombeaneni. Muulize mahitaji yake ni nini. Shiriki naye mahitaji yako pia.

**Jinsi unavyoweza kumsaidia Mkristo rafiki wako mpya zaidi ni KUOMBA!**

- Omba ulinzi wake kutoka kwa Shetani na ulimwengu.
- Omba ili akue kufikia ukomavu katika Kristo.
- Omba kwamba ataelewa kila somo na kumtii Mungu kikamilifu katika kulitumia hilo somo maishani mwake.




**Zungumza** na kiongozi wa kikundi chako kumhusu rafiki yako ambaye ni muumini mpya. Ikiwa unamjua mtu ambaye hajawa muumini, uliza kiongozi wako wa kikundi cha uanafunzi ikiwa yupo mtu mwingine ambaye unaweza kumsaidia kukua katika Kristo. Fikiria kufanya kazi na mtu ambaye ni mdogo kwako kwa mwaka mmoja au miwili. Andika jina la mtu huyo hapa:_____________________________________

Muulize mtu huyo ambaye uliandika jina lake akutane nawe peke yako kwa wiki sita ili kupitia kitabu cha *Kuanza*. Unapojiandaa kwa kila kipindi, fuata maelekezo katika sehemu hii.

**Kamilisha sehemu hii kwa kukariri 2 Wakorintho 5:17**

# KAZI

1. Kuwa na wakati peke yako na Mungu kila siku juma hili, kwa kutumia maandiko yafuatayo:

Siku ya 1: Matendo 27:1-12

Siku ya 2: Matendo 27:13-26

Siku ya 3: Matendo 27:27-44

Siku ya 4: Matendo 28:1-10

Siku ya 5: Matendo 28:11-16

Siku ya 6: Matendo 28:17-22

Siku ya 7: Matendo 28:23-31

2. Endelea kushiriki ushuhuda wako na uwasilishaji wa Injili kila wiki.

3. Endelea kupitia kitabu cha *Kuanza* na muumini mpya, kumsaidia kwenda mbele katika uhusiano wake na Yesu Kristo.

4.Ongea na kiongozi wa kikundi chako kuhusu kuendelea katika Mfululizo wa vitabu vya *Hatua kuelekea Ukomavu* kwa kusoma *Kuuathiri Ulimwengu Wako*. Agiza kutoka kwa Reach Out Youth Solutions katika www.reach-out.org au piga I -800-473-9456.

**MAMBO UNAYOHITAJI:**
**Kuanza na**
**Kuuathiri Ulimwengu wako**

# KADI ZA KUMBUKUMBU ZA BIBLIA

Kila mstari wa kumbukumbu kwenye kadi hizi umechapishwa katika toleo la New International (NIV). Mistari hiyo inalingana na sehemu mbalimbali katika kitabu hiki.

**TEMBEA NA MISTARI HII POPOTE UENDAPO**

Tumia kile kinachokusaidia zaidi:

—Zungusha mpira kwenye kadi hizo.
—Zibebe kwenye bahasha.
— Ziweke kwenye pochi lako au kijitabu cha mfuko.
—Ziweke kwenye gari lako.
—Zibebe katika Biblia yako.
—Kila siku pitia kila mstari ambao umejifunza.
—Muambie mtu aangalie maendeleo yako kila wiki.
—Tumia kila mstari katika maisha yako ya kila siku.

| | |
|---|---|
| 1. KUMJUA MUNGU<br>**Yohana 17:3**<br>Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma. Yohana 17:3 (NIV) | 6. MATOKEO YA UFUFUO<br>**1 Petro 3:18**<br>Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa (NIV) |
| 2. MADHARA YA DHAMBI<br>**Warumi 3:23, 6:23**<br>kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;…Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. (NIV) | 7. KUTUBU<br>**Marko 1:5**<br>Wakamwendea nchi yote ya Uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto wa Yordani, wakiziungama dhambi zao. (NIV) |
| 3. HUKUMU<br>**Waebrania 9:27**<br>Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu. (NIV) | 8. WATOTO DF MUNGU<br>**Yohana 1:12**<br>Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake (NIV) |
| 4. UPENDO WA MUNGU<br>**Warumi 5:8**<br>Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi (NIV) | 9. YESU ANABISHA<br>**Ufunuo wa Yohana 3:20**<br>Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami. |
| 5. UFUFUO<br>**1 Wakorintho 15:3-4**<br>Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko;… na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko. (NIV) | I0. UUMBAJI MPYA<br>**2 Wakorintho 5:17**<br>Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. (NIV) |